epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Agosti 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581764
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**TEN HAG ALIA NA MAJERUHI MAN UNITED**

UKURASA WA 2

**Kijana** afariki dunia akisafisha kisima cha mafuta, baba yake azirai

UKURASA WA 17

**Uingereza** yaahidi kumlinda Mtanzania aliyedai usalama wake uko shakani



UKURASA WA 24

**Magoma** abwagwa kortini, aamuriwa kuilipa Yanga fidia

# TRA yapata dawa kukomesha migogoro na wafanyabiashara

UKURASA 2



Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda.

UKURASA WA 21

**JULIAN ARAUJO KUONDOKA BARCELONA**



MCHEZAJI wa kimataifa wa Mexico mzaliwa wa Marekani, Julian Araujo anakaribia kuhama kutoka Barcelona kwenda...

## Waitaka INEC kuongeza udhibiti maboresho daftari la mpigakura

UKURASA 5




Wadau wa uchaguzi, wakishiriki katika mkutano wa siku moja na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), jijini Mwanza jana. **PICHA: INEC**

# Mbaroni madai ya kumbaka binti

• **Ni** waliodaiwa kutumwa na bosi wao kisa... *Endelea ukurasa 3*

MICHEZO SIMBA, YANGA HAWAJAMALIZANA UK.24 KATUNI UK.6

## Kijana afariki akisafisha kisima cha mafuta, baba yake azirai

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KIJANA Sharom Tarimo (21), amefariki dunia baada ya kuingia katika kisima cha mafuta kinachomilikiwa na kampuni ya Total Energies, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza mara baada ya uokoaji, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Msaidizi (ASF) Jeremia Mkomagi, alisema jana saa 5:23 asubuhi walipokea taarifa ya uokoaji huo, katika kituo hicho cha mafuta kilichopo mkabala na Ofisi za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema ni utaratibu wa kawaida wa kusafisha kisima hicho, kuona kama kinauwezo wa kuendelea kuhifadhi mafuta.

"Tulipokea taarifa ya uokozi wa mtu mmoja kuingia katika kisima cha mafuta kilichokuwa kinafanyiwa mahesabu, upimaji na marekebisho kama kinaweza kuendelea kufanya kazi. Tulifika na kuanza shughuli za uokozi kwa kunyonya maji yaliyokuwa yamechanganyikana na dizeli na kisha kuopoa mwili huo.

"Mwili wa Tarimo umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mawenzi," alisema Kamanda Jeremia.

Alisema kisima hicho hutumika kuhifadhia mafuta lita 40 na wakati wa kukifanyia usafi huwekwa maji.

Kutokana na tukio hilo, Mkomagi alitoa rai kwa wamiliki wa vituo vya mafuta kuchukua tahadhari za kutosha wanapofanya utaratibu wa kawaida wa usafishaji wa visima ili kuondokana na athari za namna hiyo.

Mmoja wa mashuhuda, Lucy Msami, alisema kijana huyo alikuwa na mtu mwingine (anayedaiwa ni baba yake mzazi) ambaye yeye alipatwa na mshtuko na kupoteza fahamu na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi.

"Inaonekana hakuchukua tafadhali au kuna kitu hakikwenda sawa. Ila bado wenye vituo vya mafuta wanapaswa kuongeza umakini hasa katika usafishaji wa visima vyao," alise-



Kamishna wa Uchunguzi wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Evarist Mashiba, akizungumza kwenye mkutano wa wahariri na waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi wa TRA Sikika App, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**

# TRA yapata mwarobaini kukomesha migogoro na wafanyabiashara

**Na Restuta James**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yussuf Mwenda, amesema katika kutatua migogoro ya wafanyabiashara, wakiwamo wa Kariakoo, mamlaka imeweka utaratibu wa kukutana nao mara tatu kwa mwezi ili kuwasikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero zao.

Amesema TRA imezindua APP (application) kwa ajili ya kupokea maoni, ushauri na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara na wananchi ambao yatamfikia Kamishna Mkuu moja kwa moja.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari pamoja na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa App hiyo inayoitwa 'TRA Sikika App', Mwenda alisema wameamua kukutana na wafanyabiashara katika vipindi hivyo ikiwa ni njia ya kutatua changamoto zao.

"Tutakutana nao kwa mwezi mara tatu na mimi nitakuwa ninakwenda kukutana nao ili kutatua matatizo yao na ndilo la msingi zaidi. Tunafanya hivyo," alisema.

Alisema moja ya malalamiko ya wafanyabiashara wadogo katika soko hilo ni kutotoa Risiti za Kielektroniki (EFD), kuingiza mizigo nchini kwa kuchangia kasha na hivyo mtu mmoja kulipia ushuru wa forodha.

"Tumetengeneza timu na wale wanaoigiza kwa kuchangia makasha, hii ni moja ya namna ya kutatua changamoto inayowakabili.

"Nyingine walitaka wajue makadirio ya kodi kabla hawajaagiza mzigo. Tumekubaliana tuwe na viwango vya makadirio kwa shehena mbalimbali," alisema.

Alisema bidhaa nane vikiwamo vitenge na nguo, zimeshawekewa makadirio ya ushuru wa forodha na kwamba, hivi sasa mfanyabiashara anajua kiasi atakacholipa kabla ya kuagiza.

"TRA inataka kuona Kariakoo inakuwa soko lenye ushindani mkubwa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Haipendezi kuita Soko la Kimataifa wakati watu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hawaji. Tunaamini wakija wengi tutapata kodi zaidi; na hili linawezekana," alisema.

Mwenda alisema sekta isiyo rasmi ni kubwa na kwamba, TRA inatengeneza mfumo utakaoziwezesha mamlaka zote za serikali kusomana na kurahisisha kuwatambua wafanyabiashara wa ngazi zote kuanzia wadogo.

"Tutajenga mifumo ya kodi za ndani na ya forodha. Kumekuwa na malalamiko mengi kwamba, mifumo haisomani na kutosomana kunapoteza kodi za Watanzania. Tutajenga Mfumo wa Forodha (TANCIS), ambao utazinduliwa Januari mwakani ili kuhakikisha kwamba, taarifa tunazozipata ni sahihi na zinatumika kutenda haki na kutoa uamuzi sahihi wa kodi.

"Tunaamini hii mifumo itatusaidia kujuwa wafanyabiashara ambao hawako kwenye taarifa za TRA. Tukiimarisha hii ninaamini tutaongeza tax base (idadi ya walipakodi)" alisema.

Kuhusu malalamiko ya wawekezaji katika masuala ya kodi, Mwenda alisema ameweka utaratibu wa kukutana nao, ili kusikiliza kero na maoni yao kuhusu maboresho wanayopendekeza.

Alisema ameshakutana na ujumbe wa Balozi wa China nchini, na wiki ijayo atakutana na Balozi wa Marekani, huku pia akikutana na wawekezaji wazawa.

"Tunakutana nao kujua wana changamoto zipi ili tuzitatue. Zile ambazo ziko ndani ya sheria tutazishughulikia, zilizo nje ya sheria tutaziwasilisha serikalini ili zifanyiwe kazi," alisema.

Mwenda alisema mkakati wake ni kushirikiana kikamilifu na walipakodi wote ili kutatua changamoto na kuongeza ubunifu wa kukusanya kodi.

**BANDARI**

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanakwepa kodi kuanzia bandarini kwa kutoa mizigo wakidai ni ya nje ya nchi, badala yake wanaiuza soko la ndani.

"Kitengo chetu cha ufuatiliaji wa bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi tumekiimarisha ili kuhakikisha mizigo hiyo inatolewa nchini.

"Niseme ni rahisi kudhibiti mizigo hii kwa hiyo tutaimarisha ufuatiliaji na kama kuna watumishi wetu wanashirikiana na wakwepa kodi tutawaondoa," alisema.

**SIKIKA APP**

Kuhusu aplikesheni hiyo, Mwenda alisema wafanyabiashara na wananchi wanaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kwa kuwasilisha maoni na malalamiko ya huduma za TRA.

"Hii ni moja ya njia ya kuwasiliana na walipakodi. Tutaendelea kutoa elimu ya kodi na kuboresha huduma za kodi. Ofisi zetu zitakuwa wazi kwa ajili ya kutatua changamoto zozote za kikodi," alisema.

Akizungumzia aplikesheni hiyo, Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa TRA, Emmanuel Nnko, alisema inatoa fursa kwa wananchi kuwasiliana na Ofisi ya Kamishna Mkuu na kuongeza uwazi na uwajibikaji wa mamlaka hiyo. Alisema taarifa zitakazotumwa kwenye aplikesheni zitasaidia kuongeza ushirikiano kati yake na walipakodi kwa kufahamu mahitaji yao na kuyashughulikia kwa wakati. Kamishna wa Forodha, Juma Bakari, alisema mfumo wa kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wanaochangia kasha kuingiza shehena nchini na kila mmoja kulipia, umeanza kutumika mwezi huu.

Juni mwaka huu, wafanyabiashara katika mikoa mbalimbali walifunga maduka wakilalamikia pamoja na mambo mengine, mifumo ya kikodi inayowaumiza.

Mwezi uliopita, Rais Samia Suluhu Hassan, aliunda kamati ya kupitia mifumo ya kodi kwa ajili ya kushughulikia tatizo hilo ili kuweka mazingira mazuri ya kundi hilo katika ufanyaji kazi wao. Rais Samia alitoa taarifa ya uundwa kwa kamati hiyo katika mkutano wa 15 wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) baada ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), kueleza changamoto wanazokutana nazo wafanyabiashara zikiwamo kufungiwa akaunti za benki, kuchukuliwa fedha bila utaratibu sahihi na kufungiwa mashine za kutoa risiti (EFD).

HABARI KITAIFA

# Waliodaiwa kumbaka binti mbaroni

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini linawashikilia watu wanne kati ya sita wanaodaiwa kuhusika katika tukio la binti, mkazi wa Yombo Dovya, Temeke, Dar es Salaam, aliyefanyiwa ukatili kwa kulawitiwa na kubakwa.

Aidha, jeshi hilo limesema limebaini unyama huo ulitendeka Mei, mwaka huu, eneo la Swaswa jijini Dodoma.

Limesema tayari binti huyo amepatikana na amehifadhiwa eneo salama na anaendelea kupata huduma zinazostahili zikiwamo za kisaikolojia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi Nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, watuhumiwa hao wamekamatwa jijini Dodoma na mkoa wa Pwani, huku jeshi hilo likiendelea kuwasaka wengine wawili waliojificha.

"Jeshi la Polisi linatoa taarifa ya uchunguzi wa tukio ambalo lilisambazwa katika mitandao ya kijamii kupitia picha mjongeo (video clip) kuanzia Agosti 2, mwaka huu.

"Hadi sasa uchunguzi umefanikisha kukamatwa watuhumiwa wanne kati ya sita ambao walipanga na kutekeleza uhalifu huo. Watuhumiwa hao ni Clinton Honest Damas kwa jina maarufu Nyundo, Praygod Mushi, Amini Lema na Nikson Jakson," alisema.

Misime alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea kukamilishwa sambamba na kuwasaka watuhumiwa wawili ambao bado wamejificha ili wafikishwe mahakamani.

"Kwa hawa ambao bado wamejificha kama kuna yeyote anayefahamu wamejificha kwake atoe taarifa na asipofanya hivyo, wakikamatwa wakiwa nyumbani au katika makazi yake atakamatwa na kufikishwa mahakamani," aliomba.

Misime pia alisema wamewakamata watuhumiwa wanne Dar es Salaam baada ya kukiuka sheria na kusambaza picha mjongeo wa tukio hilo katika mitandao ya kijamii ambao ni Flora Miombola, Aghatha Mchome, Madatha Jeremiah Budodi na James Nyanda Paulo.

Alisema watuhumiwa wanne wamekamatwa kwa tuhuma za kutengeneza na kusambaza taarifa za uongo mitandaoni zinazosema RIP (Rest in Peace) yaani pumzika kwa amani binti aliyebakwa na kulawitiwa akutwa amefariki. "Taarifa nyingine ya uongo inasema mama wa binti huyo amedondoka na kufariki. Watuhumiwa wawili wamekamatwa huko Arusha na wawili mkoani Dar es Salaam ambao majina yao ni Amos Lwiza, Adam Dongo, Venance Mallya na Isack Elias.

"Jeshi la Polisi lingependa kutoa onyo kwa baadhi ya watu ambao hawana mamlaka ya kufanya hivyo waache tabia ya kwenda katika eneo ambalo lilitajwa kuwa huyo binti anaishi wakimtafuta yeye na familia yake ili wawahoji au kuwaona," alisema.

Misime alisema kufanya vitendo vya aina hiyo ni kuwatweza utu wao na kuwatonesha majeraha waliyonayo mioyoni mwao.

Agosti 4, mwaka huu, katika mitandao ya kijamii kulisambaa video ikionesha namna vijana watano wakimfanyia ukatili huo binti huyo huku wakimrekodi.

Katika video hiyo vijana hao walisikika wakimtuhumu kutembea na mume wa mtu na binti huyo akisikika kuomba msamaha mtu aliyejitambulisha kama afande.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akifafanua jambo kwa Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UN), Earle Courtenay Rattray (kushoto kwake), wakati walipotembelea Shamba la Serikali la Mbegu za malisho aina ya Juncao, eneo la Vikuge, wilayani Kibaha mkoani Pwani jana. Wa (pili kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Teknolojia mpya kuongeza uzalishaji malisho mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema teknolojia ya uzalishaji wa malisho aina ya Juncao ambayo imeanza kutumika hapa nchini ni suluhisho la kumaliza changamoto za malisho ya mifugo na kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Ulega aliyasema hayo jana wakati alipouongoza ugeni kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) wakiwakilishwa na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja huo, Earle Rattray, kutembelea Shamba la Serikali la Mbegu za Malisho aina ya Juncao lililopo Vikuge, Kibaha, mkoani Pwani.

"Katika shamba hili la serikali la Vikuge kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka huu tumeshapanda majani ya Juncao ekari 21, mbegu zilizozalishwa ni kilo 178,262, huku zaidi ya wakulima 957 wakishiriki kulima majani hayo kwa hatua tofauti," alisema Ulega.

Ulega alisema kuwa teknolojia hiyo ya Juncao ni sehemu katika Programu ya TUTUNZANE MVOMERO iliyozinduliwa na serikali ambayo inahamasisha wafugaji kulima malisho katika maeneo yao, kuhifadhi mazingira na kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Waziri huyo alishukuru Umoja wa Mataifa kwa mchango wao mkubwa katika kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali wa wizara hiyo kuifahamu teknolojia hiyo ya ulimaji majani ya Juncao.

"Teknolojia hii tumeichukua kama ni suluhu ya mahitaji ya malisho katika taifa letu", alisema.

Msaidizi wa Katibu Mkuu wa UN, Balozi Earle Rattray amefurahishwa na maendeleo ya teknolojia hiyo hapa nchini, huku akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonesha utayari wa kuipokea kwa kuwa ni suluhisho kwa migogoro ya wakulima na wafugaji.

# Bashungwa atia neno uboreshaji wa daftari la kura

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amewahimiza Watanzania wenye sifa za kujiandikisha katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, kujitokeza katika vituo ili kupata vitambulisho vitakavyowawezesha kupata haki ya kuchagua viongozi katika uchaguzi ujao.

Bashungwa ambaye ni Mbunge wa Karagwe mkoani Kagera, alitoa rai hiyo jana baada ya kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Kituo cha Shule ya Msingi ya Ahakishaka, Kata ya Nyabiyonza, wilayani Karagwe.

"Tukitaka kupata viongozi wazuri hatua ya kwanza ya kufanya ni kujiandikisha kwenye daftari ili tuweze kutumia haki yetu ya kidemokrasia muda utakapofika wa uchaguzi", alisema.

Bashungwa aliipongeza Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kwa kuboresha dafrati la kudumu la wapigakura na kufanya kazi kwa weledi hali inayoimarisha demokrasia nchini.

Aidha, Bashungwa alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa kuendelea kuimarisha demokrasia nchini na kuendelea kuiwezesha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Naye, Fidelis Makata, mwandikishaji wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura katika Kituo cha Ahakishaka, alisema mchakato huo unafanyika kwa siku saba kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaoendelea unaongozwa na kauli mbiu "Kujiandikisha kuwa Mpigakura ni Msingi wa Uchaguzi Bora".

# Bil. 1.1/- kunufaisha vijana kufuga kwa tija

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekabidhi Sh. bilioni 1.1 kwa vikundi 25 vya programu ya 'Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT)' ili kufuga kwa tija.

Rais alikabidhi juzi mfano wa hundi kwa baadhi ya wanufaika wa BBT katika kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane Kitaifa yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni, mkoani Dodoma.

Baada ya kutembelea banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rais Samia alionesha kufurahishwa namna vijana wanavyoendelea kunufaika kupitia sekta za mifugo na uvuvi.

Aliwataka vijana kutumia vyema fursa zinazojitokeza ili waweze kujiinua kiuchumi na kutoa elimu kwa wenzao ambao bado hawajachangamkia fursa hizo hususan katika sekta za mifugo na uvuvi.

Rais Samia alisema serikali imejipanga kujenga uchumi jumuishi unaowainua wananchi wote na kuwawezesha kunufaika ipasavyo kupitia uwekezaji unaofanywa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema serikali imeongeza bajeti kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi ili uwekezaji huo ulete mageuzi makubwa kwa kuongeza maeneo ya umwagiliaji, matumizi ya mbolea, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, kuimarisha huduma za ugani kuboresha miundombinu ya kuhudumia mifugo pamoja na upatikanaji wa huduma za ugani, chanjo, majosho na masoko.

Rais Samia alisema serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya mifugo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na utafutaji wa masoko na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wafugaji.

Wakati Rais Samia akikabidhi mfano wa hundi yenye kiwango hicho cha fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema fedha hizo ni mkopo wenye masharti nafuu na kwamba, serikali itaendelea kuitoa kwa mwaka huu wa fedha.

Waziri Ulega akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo, alisema kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, wizara imetengewa bajeti ya Sh. bilioni 465 ambayo ni maradufu ya bajeti iliyokuwa ikipata awali, ambazo zitawezesha kutatua changamoto za wafugaji na wavuvi.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha, serikali imeandaa kampeni kubwa ya kitaifa ya chanjo kwa ajili ya mifugo pamoja na kuitambua mifugo hiyo, ili kuhakikisha mifugo inakuwa na afya bora na kuleta tija kwa mfugaji.

Waziri Ulega alisema imepanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya boti za uvuvi zisizopungua 450 na vizimba 900 kwa ajili ya kufugia samaki, ili kukuza sekta hiyo kwa kuchangia pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.



Mchuuzi wa fedha, akizipanga wakati akisubiri wateja ambao asilimia kubwa ni makondakta wa daladala, katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. Noti ya 1,000/- inachenjiwa kwa 700/- hadi 800/-. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bunge lakunwa maendeleo bomba la mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, imeipongeza serikali kwa kutekeleza miradi inayoleta mageuzi ya kiuchumi katika sekta mbalimbali.

Wakati wabunge hao wakitoa pongezi hizo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, amesema ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta hadi sasa umefikia asilimia 39.2.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti walitoa pongezi hizo jana walipokuwa wakikagua utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika kituo kitakachotumika kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda. Kutokana na umuhimu wa mradi huo, wabunge hao waliahidi kuzidi kuupa msukumo kutokana na umuhimu wake katika mageuzi ya kiuchumi.

Baada ya kukagua kituo hicho Chongoleani mjini Tanga, Mwenyekiti wa Kamati, Oran Njeza, alisema wameona mradi wa EACOP una umuhimu kiuchumi, hivyo wataendelea kuupa msukumo mkubwa ili ukamilike kwa wakati.

Kamati hiyo imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mabadiliko ya kiuchumi anayoyafanya kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama wa EACOP, ambayo inaendana na jinsi dunia inavyokwenda kwa sasa.

"Mradi mkubwa kama wa EACOP haukutegemewa kufanyika kwenye nchi za kiafrika lakini maono ya viongozi wakuu wa Uganda na Tanzania yamesababisha mradi huu kufanyika ili kuwezesha mafuta sasa kusafirishwa kwa njia ya mabomba ambayo pia yanasaidia katika ulinzi wa mazingira," alisema Njeza.

Aidha, kamati imeitaka Wizara ya Nishati kuweka kipaumbele katika ujenzi wa mabomba yatakayosafirisha nishati za aina mbalimbali kama vile gesi na mafuta, hivyo kuifanya Tanzania kuwa kituo cha usafirishaji wa nishati hizo barani Afrika. Kamati pia imeliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza nguvu ya kuutangaza mradi huo ili wananchi wafahamu jinsi serikali inavyoendelea kutekeleza miradi yake.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, alisema EACOP ina faida mbalimbali katika mkoa huo ikiwamo kutoa ajira takriban 900, kuongeza mzunguko wa fedha, kuongeza fursa za biashara ikiwamo katika kituo cha kupokelea, kuhifadhi na kusafirikisha mafuta kilichoko Chongoleani Tanga, kuuza rasilimali kama vile simenti na kupata mapato mbalimbali kupitia ushuru.

Alitilia mkazo masuala ya afya na usalama mahali pa kazi katika miradi mbalimbali nchini na kuipongeza EACOP kwa kutekeleza suala hilo kwa ufanisi. Kwa zaidi ya saa zaidi milioni mbili waliyofanya kazi, alisema hakuna ajali iliyotokea kwenye maeneo yao ya kazi. Awali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio alisema mradi wa EACOP ni wa kielelezo na kimkakati kutokana na faida zake mbalimbali ikiwamo kuongeza mapato ya nchi katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji kwa Sh. trilioni 2.3, kutoa ajira kwa watanzania ambapo mpaka leo umeajiri takriban wananchi 7,584 huku ajira hizo zikitarajiwa kuongezeka.

Aliongeza kuwa kampuni 146 za kitanzania zimehusika kutoa huduma mbalimbali kwenye mradi na kunufaika kwa takriban Dola za Kimarekani milioni 246 na pia mradi umewezesha kufanyika kwa ununuzi wa Dola za

Marekani milioni 462 na vijana wa kitanzania kupata mafunzo ya teknolojia mbalimbali. Ujuzi huo watautumia kwenye miradimingine ya ujenzi wa mabomba kuelekea Kenya na Zambia. Dk. Mataragio alisema mradi unaendelea vizuri na sasa umefikia asilimia 39.2 huku baadhi ya kazi zikikamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa kiwanda cha kuwekea mabomba mfumo wa kuhifadhi joto cha Sojo ukifikia asilimia 90. Pia alisema katika eneo la Chongoleani, mradi umefikia asilimia takriban 40 na kubainisha kuwa mradi unatarajiwa kukamilika Juni, 2026.

# DC aunda kamati mapambano kamari, shisha

**Na Romana Mallya**

SIKU chache baada ya gazeti hili kuripoti kuhusu kushamiri kamari na uvutaji shisha katika makazi ya watu maeneo ya Mwananyamala, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya hiyo, Saad Mtambule, ameunda kamati za maadili kuanzia ngazi za mitaa na kata ili kukabiliana navyo.

Julai 20 na 21, mwaka huu, gazeti hili liliripoti kushamiri kwa kamari na uvutaji wa shisha katika makazi ya wananchi, unaohusisha watoto na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilitia neno katika hilo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM) Amos Makalla, Julai 17, mwaka huu, akiwa ziarani mkoani Dar es Salaam, aliagiza mkuu wa wilaya hiyo na timu yake kuandaa majibu ya kero za wananchi zikiwamo hizo zinazolalamikia na kabla ya kumaliza ziara yake taarifa kamili waikabidhi.

Jumatano, ikiwa ni siku ya 23 tangu agizo la Makalla kutolewa, Mtambule alitangaza kuunda kamati za maadili kuanzia ngazi za mitaa na kata ili kukabiliana na vitendo vya ukatili vikiwamo hivyo.

Akizungumza katika mkutano uliojumuisha viongozi wa dini na wenyeviti wa mitaa, kata na taasisi za kijamii zinazojishughulisha kupinga vitendo vya ukatili, Mtambule alisema hali katika mitaa wilayani humo si ya kuridhisha.

Alisema hali si ya kuridhisha kutokana na vijana wengi kujiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya, ulevi, ukahaba na uchezaji kamari.

"Tumeona kuna kina dada maarufu 'dada poa' baadhi ya mitaa yetu wanafanya biashara ya ukahaba. Tuna vijana wetu wa kiume wanafanya biashara ya ushoga, tunao watoto wetu wanaofanyiwa ukatili wa aina mbalimbali wanabakwa na wanalawitiwa.

"Lakini pia tumeona kuna vijana ambao wameingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya, uchezaji wa kamari uliopitiliza, unywaji wa pombe uliopitiliza, na uhalifu mwingine wa udokozi wa hapa na pale,"alisema.

Alisema kwa kuangalia hayo yote, sababu kubwa ni wanaiona inachangiwa na malezi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Mtatiro Kitinkwi, alisema wahalifu wana tabia moja ya kuona kama adhabu haijatolewa kunakuwa na tabia ya kurudia makosa.

"Adhabu ikitolewa na jamii ikaona wahalifu wakaona basi tunakuwa tumepunguza makosa na uwezekano wa kutokea tena," alisema.

Paroko wa Parokia ya Watakatifu Mashahidi wa Uganda, Magomeni, Padri Christian Likoko, alisema kupitia mkutano huo wamejiwekea malengo mbalimbali kama wilaya chini ya Mkuu wa Wilaya kukabiliana na vitendo hivyo.

# Simbachawene aagiza kukamilishwa ajira za walimu na madaktari

**Na Mwandiashi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameagiza kukamilika kwa mchakato wa ajira mpya za walimu na madaktari ili kupunguza pengo la watumishi katika kada hiyo,

Simbachawene alitoa maagizo hayo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Wangi, Jimbo la Kibakwe kwenye mkutano wa hadhara wakati wa uzinduzi wa Shule ya Sekondari Wangi.

"Ninamuelekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kushirikiana na Katibu Mkuu TAMISEMI (ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ili kuhakikisha shule zote mpya na vituo vya afya nchi nzima vilivyokamilika vinapangiwa walimu na madaktari mtawalia.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametoa ajira zaidi ya 12,000 kwa sekta za afya na elimu, hivyo hatuna budi kuhakikisha wanapangwa vizuri ili wananchi wapate huduma ipasavyo," alisema.

Aidha, Simbachawene aliwaomba wananchi wa kata za Wangi na Wotta kushukuru kwa maendeleo ambayo yameletwa mathalani ujenzi barabara, shule na vituo vya afya kwa lengo la kurahisisha maisha kwa wananchi.

Kutokana na jitihada hizo za serikali katika kuwaletea maendeleo, aliwaomba wananchi wa Kibakwe katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kukichagua Chama Cha Mapinduzi (CCM) hasa Rais Samia na yeye kuendelea kuwa mbunge na madiwani wa chama hicho ili waendelee kutekeleza maono waliyo nayo badala ya kuanza upya.

Simbachawene anaendelea na ziara katika Jimbo la Kibakwe na amefanya mikutano ya hadhara katika kata za Wotta na Wangi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.




Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani sh. milioni 354 kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege (kushoto), iliyotolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ikiwa ni fidia kwa wakulima wa zao tumbaku walioathirika na mvua za mawe katika msimu wa kilimo uliopita kwenye mikoa tofauti nchini, wakati kilele cha maonesho ya wakulima nanenane, jijini Dodoma juzi. Fidia hiyo, inatokana na huduma ya bima ya kilimo inayotolewa na benki hiyo kwa kushirikiana Shirika la Bima la Taifa (NIC). Wengine ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi (wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Kaimu Mkeyenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waitaka INEC kuongeza udhibiti maboresho daftari la mpigakura

**Na Vitu Audax,** MWANZA

WADAU wa Uchaguzi mkoani hapa wameiomba serikali kupitia Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kuongeza udhibiti na usimamizi makini katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Lengo ni kuondoa shaka na viashiria vya ukiukwaji wa taratibu katika mchakato huo.

Wakizungumza jana nje ya mkutano wa INEC na wadau wa uchaguzi mkoani humo, wadau hao walisema hayo baada ya kueleza kubaini baadhi ya mapungufu katika mchakato huo katika maeneo yalipofanyika maboresho.

Mwakilishi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Abas Mayala, alisema pamoja na mambo mengine, wamebaini ukiukwaji wa Sheria ya Uchaguzi Na. 7, kifungu kidogo cha nne cha sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kinachokataza viongozi na makada wa vyama kisiasa kushiriki katika kuandikisha daftari hilo.

"Katika mikoa ya Katavi, Kigoma na maeneo mengine tumeona kuwapo kwa upungufu mbalimbali ikiwamo ya viparata, kuharibika kwa mashine, vilevile tumeona makada pamoja na viongozi wa vyama wakishiriki kama maofisa wa uandikishaji jambo linaloleta madhara kwa upande wa vyama vingine," alisema Mayala.

Alisema katika eneo la Kabindi mkoani Kigoma, baadhi ya mawakala wa chama hicho wanadaiwa kunyimwa vitabu vinavyotoa maelekezo ya kusimamia kama mawakala hivyo kuiomba tume hiyo kuongeza umakini katika maboresho hayo kwa kudhibiti viashiria hivyo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, Michael Lushinge, alisema vyama vya kisiasa vina jukumu la kuwafikia wananchi wote na kuwaelimisha kuhusu ushiriki wao katika maboresho hayo, ili kufikia lengo na kumfikia kila mtanzania mwenye sifa ya kujiandikisha bila kujali itikadi za vyama wanavyoyosimamia.

Mwakilishi wa Wanawake kutoka Wilayani Ukerewe, Sophia Donald, aliiomba serikali kupitia tume hiyo kuongeza muda wa uboreshaji wa daftari hilo hasa katika maeneo yenye jiografia sisizofikika kwa urahisi ili kuwasaidia wanawake na watanzania kwa ujumla kushiriki ipasavyo.

"Kwa Ukerewe tunavyo visiwa zaidi ya 30 ambako kati ya hivyo, visiwa 15 vinakaliwa na watu. Tatizo kubwa ni ufikiwaji wa visiwa hivyo pamoja na shughuli za wananchi, hivyo kwetu siku saba ni kidogo zingeongezwa ili wananchi wafikiwe," alisema.

Akifungua Mkutano huo, Mwenyekiti wa INEC, Jaji wa Rufani Jacobs Mwambegele, alisema kwa sasa tume hiyo inaendelea na jukumu la uboreshaji wa daftari hilo kwa mujibu wa Katiba ya Mwaka 1977, Ibara ya 74 (4) pamoja Sheria ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge pamoja na Madiwani kwa Tanzania Bara iliyofanyiwa marejereo mwaka 2024 kifungu cha 16(5).

Jaji Mwambegele aliwaondoa hofu wadau hao kuwa vifaa vya uboreshaji vimefanyiwa maboresho na kuwa kazi inafanyika kwa ufanisi na kuzingatia sheria na taratibu.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 168 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 kadi za mpigakura zilizotolewa mwaka 2015 na 2020 zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni halali na zitaendelea kutumika katika uchaguzi ujao, hivyo mchakato hauwahusu wenye kadi hizo, "alisema Jaji Mwambegele.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC na Katibu wa Tume, Ramadhan Kailima, alisema kwa mkoa wa Mwanza wanatarajia kuwa na wapigakura wapya 190,131 sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ya wapigakura 1,845,816 walioko sasa.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Ratiba Ligi Kuu imetoka, klabu tunataka ushindani

**WIKI** hii tumeshuhudia matukio mbalimbali katika soka kwa hapa nyumbani na kuwapa burudani na furaha mashabiki wa mchezo huo pendwa.

Baadhi ya matukio hayo ni pamoja na tuzo za wanamichezo bora waliofanya vizuri msimu uliopita wa 2023/2024, tukashuhudia klabu ya Yanga ikifanya vizuri kwenye tuzo hizo.

Lakini baadaye kukawa na matamasha ya klabu kubwa hapa nchini, Simba na Yanga ambayo yalipishana kwa siku moja na kuteka hisia za mashabiki wa timu hizo.

Kama hiyo haitoshi, baada ya matamasha hayo sasa ikafuatia michezo miwili ya nguvu ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii ikiwa ni kiashirio cha kufunguliwa kwa pazia la Ligi Kuu msimu wa 2024/2025.

Michezo hiyo ni ile ya Simba dhidi ya Yanga uliochezwa kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na ule wa Coastal Union dhidi ya Azam FC uliochezwa kwenye uwanja wa New Aman Complex, Zanzibar.

Siku moja baadae, Bodi ya Ligi Kuu ikatangaza ratiba ya msimu mpya wa Ligi wakizipanga Simba na Yanga kukutana Oktoba 19 kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza.

Kutokana kwa ratiba hi,i niwazi sasa tunaanza msimu mpya, msimu uliosubiriwa kwa hamu kubwa na mashabiki wa soka baada ya msimu wa 2023/2024 kumalizika Mei mwaka huu.

Hii ni ishara ya taa ya kijani kwa klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu msimu huu mpya kuwa sasa ziwe tayari.

Kimsingi mashabiki wa soka na wapenzi wa mchezo huo wanatarajia kuona Ligi yenye upinzani mkubwa, na yenye kuleta msisimko zaidi.

Tunavishauri vilabu vyetu vijipange na vipambane kutoa ushindani kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa ligi na isiwe ligi ya timu mbili au tatu wakati kuna timu 16 zinazoshiriki.

Kila timu ilikuwa na muda wa kutosha wa kujiandaa kabla ya filimbi ya kuashiria kuanza msimu mpya wa Ligi, hivyo hatutarajii visingizio vyovyote kwenye kushindwa kwao.

Zipo timu zenye 'msuli mkubwa' ambazo zilienda kufanya maandalizi yao nje ya Tanzania, lakini zipo zile ambazo zilitoka mikoani mwao na kwenda mikoa mingine kuweka kambi.

Wadau wa soka tunataka kuona Ligi kweli ikipigwa, tunataka kuona kila msimu ligi inakuwa ngumu zaidi ya msimu uliopita, hii ndio itafanya soka letu lizidi kwenda mbele.

Klabu ziache zisingizio visivyo na mashiko pale wanapofanya vibaya, zijikite kwenye kutambua makosa na kuyafanyia kazi haraka ili kuendelea kufanya vizuri.

Kwa timu zilizopanda daraja nazo zitambue zinaweza kufanya vizuri kama zitapambana na kufuata misingi ya ushindani, haitapendeza kuziona zikichukua miaka mingi kupanda daraja, lakini zikatumia msimu mmoja tu kushuka daraja, waige kwa Mtibwa Sugar ambao wamekaa kwa miaka zaidi ya 23 bila kushuka daraja tangu ilipopanda kwa mara ya kwanza.

Kwa ujumla tunazitakia kila la heri timu zote kwenye msimu huu mpya ambao unaanza Ijumaa ijayo, tunatarajia ushindani mkubwa kutoka kwao, kila la heri kwa msimu mpya 2024/2025

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Bora wasemaji 'makomediani' kuliko wanaodhalilisha watu

**WIKI** ilikuwa ya moto sana kwenye mitandao ya kijamii na vipindi vya michezo, hasa baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo kuja na maelezo ya kuwachukulia hatua wasemaji wa klabu au Maofisa Habari ambao wanachekesha, badala ya kuwahabarisha wanamichezo nini kinaendelea katika klabu zao.

Ofisa Mtendaji Mkuu yeye akataka wasemaji kujikita kwenye kuelezea timu zao 'kavu kavu' bila kuonesha chembe ya ucheshi.

Jambo hili limezua mjadala sana kwa wanamichezo, na hata ambao si wanamichezo, yaani watu wa kada nyingine wakijiuliza kama Bodi ya Ligi itawachukulia hatua watu hao, itakuwa inatumia vigezo gani kutambua kama msemaji huyo amechekesha, au waaandishi wa habari na wasikilizaji wamecheka bila yeye kuchesha.

Sijajua sana lengo hasa ilikuwa ni nini, au alikuwa anamaanisha haitakiwi kabisa kwa Ofisa Habari kuchekesha au kufanya mizaha, lakini nadhani binafsi naona kulikuwa na mambo mengi muhimu kwa Bodi ya Ligi kutolea ufafanuzi kuliko hilo ambalo halina tija.

Kwanza kabisa ucheshi au kuchekesha ni kipaji, wala siyo kila mtu anaweza kuwafurahisha watu, si kwa Maofisa Habari na Wasemaji, bali hata kwa Wanasiasa.

Sasa sidhani kama kweli Kasongo alikuwa anazuia kipaji cha mtu. Mwingine hata asipochekesha, jinsi anavyoongea tu na kuwasilisha taarifa au ujumbe wake watu anajikuta wanacheka.

Nitoe mfano kwa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, ni kiongozi ambaye Dunia nzima inamfahamu kuwa ni mmoja wa viongozi bora kuwahi kutokea.

Amefanya mambo mengi mazuri ambayo yameendelea kukumbukwa vizazi hadi vizazi. Lakini ukimsikiliza kwenye hotuba zake zote, hakuna hata moja ambayo Waandishi wa Habari na wengine wanaomsikiliza'hawajavunjika mbavu.'

Ni hotuba bora kabisa zenye msisimko, hekima na busara za hali ya juu, lakini karibuni zote zimebebwa na ucheshi, kiasi kwamba watu wanaweza kukaa wanasikiliza hata masaa manne bila kuchoka kumsikiliza au mtu kusinzia.

Rais wa awamu ya tano, John Magufuli, naye alikuwa na aina fulani ya hotuba za ucheshi, ambazo ziliwaacha wasikilizaji wakifurahi na kucheka, huku wakiendelea kumsikiliza.

Hii ni mifano michache ya Wanasiasa ambao wana uwezo huo, hiki ni kipaji na si kila mtu anaweza.

Hata kwa watu wa kawaida, utakuta kuna mtu ukikaa naye unafurahi tu kutokana aina yake ya mazungumzo na uwasilishaji wa maneno yake, halafu mwingine hana kipaji hicho.

Kwa wasemaji, kuna mtu anaitwa Thobias Kifaru, Masau Mbwire, Ahmed Ally na wengineo ni baadhi ya wasemaji wanaoonekana wana vipaji vya kuwasilisha taarifa zao kwa namna ya ucheshi na wamekuwa hivyo kwa miaka mingi na watu wamekuwa wakifurahi wanapowasikia wakiongea. Hilo huwezi kuondoa kwa sababu ni kipaji kutoka kwa Mungu. Hata ukiwaiga huwezi. Lakini sijawahi kusikia wakimdhalilisha au kumsema mtu kwa kuukweza utu wake kwa sababu ya mpira.

Tujiulize, kama hata viongozi walikuwa watoa hotuba zao zenye ucheshi ndani yake, iweje kwenye mpira tu ambao ni burudani ndiyo ikatazwe?

Mimi nadhani Kasongo angetuambia kuwa anapiga marufuku Maafisa Habari ambao badala ya utani, wanadhalilisha klabu zingine kwa kuchafua 'brandi' kwa kisingizio cha utani wa jadi, kumshambulia mtu binafsi kwa maneno au taasisi.

Utani, masihara, ucheshi ndivyo vinavyonogesha mpira wetu, hivi vingeachwa tu, na badala yake Bodi ya Ligi ingejikita kwa wale wenye lugha za zenye ukakasi kwa wenzao, kuvunjiana heshima, vitu ambavyo tumekuwa tukiviona.

Na hili lifanyike si kwa kuchagua au kumuangalia mtu usoni, adhabu itolewe kwa yoyote atakayefanya, ila hili la 'vichekesho', sidhani kama lina maana sana.

Bodi simamieni misingi ya uadilifu wa heshima, adabu, hivi ndivyo muhimu zaidi kuliko hilo la ucheshi wa maneno.

# Mbunge aomba huduma mpaka Kabanga saa 24

**Na Judith Julius,** NGARA

MBUNGE wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, ameiomba serikali kuboresha mpaka wa Kabanga ili ufanye kazi kwa saa 24 kama ilivyo kwa mpaka wa Rusumo.

Ruhoro alitoa rai hiyo juzi kwenye mkutano uliohudhuriwa na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Emmanuel Nchimbi, uliofanyika kwenye viwanja vya Posta mjini hapa.

Mbunge huyo aliiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupeleka makontena na kufungua ofisi kwenye mpaka wa Mugoma ili uanze kufanya kazi.

Ruhoro alisema huku akisisitiza kuwa ni muhimu kwa jambo hilo kutekelezwa ili eneo la Mugoma liwe na kituo cha forodha kitakachoweza kukusanya mapato.

Nchimbi pia alisema amefurahishwa sana na wananchi wa wilaya ya Ngara mkoani Kagera kwa kutambua umuhimu wa kuwa na vitambulisha vya taifa.

Katibu Mkuu huyo alisema kuwa amelichukua suala hilo kama changamoto na kulipeleka mahali husika ili liweze kutatuliwa haraka.

Nchimbi alisema suala la mpaka wa Kabanga kufanya kazi saa 24 ni suala linalohitaji yeye kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje kwani jambo hilo linahusisha nchi za Tanzania na Burundi.

Alibainisha kuwa watakapolifikisha huko na wakakubaliana vema, anaamini mpaka huo utakuwa ukifanya kazi saa 24 kwa maendeleo ya mataifa yote mawili, akisisitiza kuwa yataweza kunufaika vizuri kupitia biashara.

Aliongeza kuwa katika kuelekea kipindi cha uchaguzi, wananchi wanapaswa kuangalia kiongozi anayekubalika na mwenye weledi, ambaye pia anaweza kushirikiana na jamii kuleta maendeleo katika eneo hilo.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Hamad Abdalah akizungumza kuhusu utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo, mbele ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi (kushoto), katika ofisi za shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ndejembi ataka ujenzi nyumba gharama nafuu

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, ameitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuweka mikakati thabiti itakayoliwezesha shirika kujenga nyumba za gharama nafuu ambazo watanzania wenye kipato cha chini watamudu kuzinunua.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na menejimenti na wafanyakazi wa shirika hilo, kuhusu mipango mikakati ya kulifanya kuendelea kutengeneza faida.

"Shirika linaenda vizuri linaingiza faida vizuri na mkurugenzi amelinyoosha shirika, ila tusisahau malengo ya NHC lilipoanzishwa mwaka 1962, yalikuwa kuwapa makazi watanzania, kwa hiyo tusiwasahau katika mipango mikakati yetu," alisema baada ya kutembelea shirika hilo.

"Maono ya Baba wa Taifa (Mwalimu Julius Nyerere) yalikuwa ni kuhakikisha tunawawezesha watanzania kufikia ndoto zao za kumiliki nyumba kwa kuwajengea ambazo watamudu kuzinunua. Tuhakikishe nyumba zenyewe ziwe na viwango bora na kuwa maeneo yanayofikika siyo nje ya miji sana," alisema.

Ndejembi aliitaka NHC kuhakikisha miradi inakuwa na thamani ya fedha kwa kuongeza ubora katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku ikiwamo kusimika mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alitaka hata wanaponunua ardhi, wahakikishe wananunua kwa thamani ya wakati huo na kuachana na madalali ambao wanaweza kuwauzia kwa gharama ambayo siyo ya soko na kulipa hasara shirika hilo.

"Kuwe na gharama halisi kwenye ununuzi wa ardhi, msije kukuta mnauziwa kwa gharama kubwa sana kutokana na watu kupandisha gharama kwa maslahi yao binafsi.

"Ila mmejitahidi sana ninawapongeza kwa miradi mingi kama ule wa Samia Housing wa Kawe nyumba 5,000 ni nyingi sana," alisema.

Ndejembi alilitaka shirika hilo pia, kuendelea kujenga nyumba za kupangisha na kuuza katika maeneo mengi nchini hasa ambayo wanaona watapata faida kwa uwekezaji watakaoufanya.

Mkurugenzi Mtendaji wa NHC, Hamad Abdallah, alisema mtaji wa NHC umeendelea kukua na kwa sasa umefikia hadi Sh. trilioni 5.16, ikilinganishwa na mwaka uliopita ulikuwa Sh. trilioni 5.04.

Alitaja moja ya sababu za ukuaji wa mtaji kuwa ni kutokana na kukamilika kwa miradi ya ujenzi na thamani ya mali za shirika inayoongeza faida ya Sh. bilioni 28.6, wakati fedha zilizokusanywa kutokana na uuzaji wa nyumba mpya zilifikia Sh. bilioni 13.1.

Abdallah alisema kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, NHC ilipanga kupata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 28 na katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024, shirika limepata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 42.2, sawa na asilimia 147 ya malengo.

Alisema shirika limefanikiwa kulipa kodi mbalimbali za serikali zinazofikia Sh. bilioni 30.2 katika kipindi cha Julai 2023 na Juni 2024.

Abdallah alisema shirika linaendelea kutafuta ardhi ya gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini na kutumia teknolojia inayopunguza gharama za vifaa vya ujenzi.

Alisema NHC inaendelea kuwasiliana na mamlaka za maji, umeme na barabara ili kuweka miundombinu katika maeneo ya ujenzi kama mkakati wa kupunguza gharama za ujenzi.

# Usafiri wakwamisha kesi ya unyang'anyi kutumia silaha

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeahirisha kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayowakabili waliokuwa askari polisi wanne na wenzao wawili, kutokana na mshtakiwa mmoja kushindwa kufikishwa mahakamani.

Sababu kuu ya mshtakiwa kutokufikishwa mahakamani ni changamoto ya usafiri wa Jeshi la Magereza. Washtakiwa hao ni aliyekuwa Koplo Ramadhani Tarimo (42) maarufu kama Rasta, Koplo Majid Abdallah (35), Koplo Stella Mashaka (41), mkazi wa Railway, Ashraf Sango (31) na Emmanuel Jimmy (31), wote wakazi wa Dar es Salaam. Wakili wa Serikali, Neema Moshi, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Franco Kiswaga kuwa kesiililetwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa na pia wana shahidi mmoja. Hata hivyo, alidai kuwa mshtakiwa wa tatu (Stella) hakufikishwa mahakamani kwa sababu ya changamoto ya usafiri, hivyo kuomba ahirisho.

Kesi imeahirishwa hadi Agosti 23,2024 na Hakimu Kiswaga alisema kama itawezekana siku hiyo walete mashahidi wawili.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo, Agosti 28, 2023, katika eneo la Kurasani, karibu na Ofisi za Uhamiaji, lililoko Wilaya ya Ilala, ambapo siku hiyo ya tukio, washtakiwa kwa pamoja waliiba Sh. milioni 90 kutoka kwa Grace Matage. Inadaiwa kabla na baada ya kufanya wizi huo, walimtishia Grace kwa bunduki ili waweze kujipatia fedha hizo bila kikwazo.

# Pinda ahimiza ulaji mboga na matunda

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amewashauri Watanzania kujenga utamaduni wa kula mboga na matunda kwa ajili ya kuondokana na tatizo sugu la utapiamlo nchini.

Pia amesema haipendezi kuona nchi ina mboga na matunda ya kutosha lakini kuna utapiamlo miongoni mwa wananchi.

Pinda alisema hayo juzi wakati akifunga Maonesho ya 30 ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Mashariki yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Tungi nje kidogo ya Manispaa ya Morogoro.

Alisema suala la utapiamlo linatokana na tatizo la watu kula chakula cha kujaza tumbo tu bila kuzingatia lishe ambapo Rais Samia ameunda baraza la ushauri la kilimo ambalo litasaidia kupiga hatua katika maendeleo ya kilimo na kutokomeza utapiamlo nchini.

Alisema baraza lenye mipango bora likianza litachukua nafasi kubwa kwa vijana kwa kutoa ajira na kupunguza suala la ukosefu wa ajira nchini.

Aidha, alisema baraza hilo pia litasisitiza namna ya kutumia rasilimali zilizopo shambani na kujiepusha na ulaji wa nyama nyekundu hovyo na kuondokana na matatizo ya magonjwa ya shinikizo la damu na figo.

Alisisitiza kuwa wajawazito kutumia lishe ili kuzaa watoto wenye afya na wamama kupata maziwa bora yatakayowakuza vyema watoto na kufanya nchi kuwa na vizazi bora kwa manufaa ya sasa na baadae.

Waziri mkuu huyo aliwataka wakazi wa Morogoro na Kanda ya Mashariki kwa ujumla kutumia tunu ya vyuo vikuu vingi vilivyopo katika kutekeleza tafiti zilizopo kikiwemo Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na kuwa vichwa katika kusimamia shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi. Hata hivyo, aliziagiza halmashauri za miji na wilaya kuwa ndio kitovu cha maendeleo kupitia mfuko wa asilimia 10 na kusaidia kuibua vikundi vya vijana, wenye ulemavu na wanawake na kuvifuatilia na kufanya urejeshwaji mzuri. "Nimetembelewa kila banda nakuona wapo wajasiriamali mmoja mmoja wengine wameshona viatu, wakiwemo wenye ulemavu na kadhalika, naomba wakusanywe kwa ajili ya kupata mikopo," alisema.




Wanafunzi wanaotarajia kwenda kusoma nje ya nchi wakiwa na wazazi wao, wakimsikiliza Mkurugenzi wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, kabla ya kugawa nyaraka na Visa katika ofisi za GEL Chang'ombe, Dar es Salaam jana kwa wanafunzi zaidi ya 100 wanaotarajiwa kwenda nje ya nchi kwa masomo kuanzia wiki ijayo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Madaktari bingwa kufanya upasuaji magoti na nyonga

**Na Joseph Mwendapole**

DAKTARI bingwa wa upasuaji wa magoti na nyonga kutoka hospitali maarufu duniani ya YASHODA ya Hyderabad, India, Dk. Ram Reddy na wenzake, wanatarajiwa kuwasili nchini mwezi huu kutoa matibabu ya upasuaji wa kibingwa wa magoti na nyonga.

Madaktari hao watafanya upasuaji huo kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa upasuaji wa viungo hivyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili - Tawi la Mloganzila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Global Medicare, ambao ni mawakala wa tiba utalii nchini, Abdulmalik Mollel, alisema madaktari hao watafanya upasuaji wa kibingwa katika kuanzia Agosti 26 hadi 28, mwaka huu.

Mollel alisema madaktari hao bobezi watashirikiana na madaktari bingwa wazawa kwenye kambi hiyo kwa lengo la kuwajengea uwezo madaktari wa ndani kwa kubadilishana uzoefu ambao utawapa ujuzi zaidi ambao utawawezesha kufanya upasuaji kama huo hata baada ya kuondoka kwa daktari huyo mgeni.

"Mwaka jana tulifanya kambi kama hii ya upasuaji na ilikuwa na mafanikio makubwa sana kwa sababu kulikuwa na zaidi ya watu 2,300 waliokuwa wanahitaji huduma hiyo. Madaktari wetu walifanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wale wa nje na tunatarajia daktari huyu bingwa na mbobezi na wenzake, watawafanyia watu wengi watakaojitokeza mapema na kufanyiwa uchunguzi wa awali," alisema.

Baada ya uchunguzi, alisema wale watakaogundulika wanahitaji matibabu hayo ya kibigwa ya upasuaji watafanyiwa.

Alisema kwa muda mrefu Watanzania wenye matatizo ya afya walikuwa wakienda nje ya nchi kwa matibabu lakini baada ya serikali kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya, wamekuwa wakitibiwa nchini.

Mollel alisema serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye vifaa tiba kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa kama iliyoko kwenye mataifa makubwa duniani na imesomesha wataalamu bobezi wa fani mbalimbali kwenye tiba. "Tanzania kwa sasa ina vifaa vya kisasa vya kutosha na wataalamu bobezi kama walioko India na kwingineko kwa hiyo sasa ni muda mwafaka madaktari bobezi wa nje waje hapa nchini kujengeana uwezo (Capacity building) na wenzao wa ndani ambao wamekuwa wakifanyakazi kubwa sana kwa ajili ya Taifa," alisema Mollel.

Alisema huduma za madaktari wabobezi zinazopatikana nchini zimewavutia watu wengi wa nchi jirani kuja kutibiwa badala ya kwenda nchi za nje kufuata tiba kama hiyo na hutumia muda mwingi na gharama kubwa.

"Kuja kwa madaktari hawa wabobezi ni jambo jema sana kwa sababu madaktari wetu watachukua zile teknolojia ambazo zitakuwa hazijafika nchini na sisi kama tuna ujuzi ambao tumewazidi wanachukua na kwa uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya afya Tanzania sasa ni kitovu cha utalii tiba kwa nchi za Afrika Mashariki na kusini mwa jangwa la sahara.

"YASHODA ni miongoni mwa hospitali kubwa duniani inayopatikana India yenye vitanda 4,000 kwa hiyo inafanya vizuri sana. Mei, 2022 ujumbe wa madaktari bingwa wa Tanzania walikwenda kujifunza wana kitu gani tofauti na hivi vilivyopo nchini. Tulijifunza wana mazingira gani yanayosababisha watu duniani kupendelea kwenda kutibiwa kwao," alisema.

Pia alisema lengo lilikuwa kujifunza yale ambayo yamewafanya wawe bingwa kwenye utalii tiba duniani na kuja kutekeleza nchini yale ambayo wameyafanya yakawapa sifa ya kuwa kitovu cha utalii tiba na kupata wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

# RC awapa kibarua maofisa tarafa, kata

**Na Gideon Mwakanosya ,**
SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahamed Abbas Ahamed, amewataka maofisa tarafa na watendaji wa kata mkoani Ruvuma, kusikiliza na kutatua kero za wananchi ili kupunguza au kumaliza matatizo yaliyoko kwenye jamii.

Aidha, wamesema kutokuwajibika kwa viongozi hao kumeathiri utoaji wa huduma kwa wananchi wa ngazi zote.

Kanali Ahamed aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa tarafa na watendaji wa kata yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Alisema changamoto zinazotokea kwenye maeneo yao ya kazi ni pamoja na kutozingatia sheria, kanuni na taratibu katika utendaji kazi wa kila siku.

Alizitaka baadhi ya changamoto ni kuwapo kwa migogoro ya kiutendaji kati ya maofisa tarafa, watendaji wa kata,wataalamu na viongozi na wataalamu wengine katika ngazi hizo.

Changamoto zingine, kwa mujibu wa Kanali Ahmed ni ufuatiliaji na usimamizi usioridhisha wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye ngazi za msingi, kutitatuliwa kwa wakati kero za wananchi pamoja na wadau wengine katika ngazi za msingi, kutokuwa na uwelewa katika baadhi ya sera,sharia na miongozo wanayotakiwa kusimamia na kuitekeleza.

Pia alisema kukosa ubunifu kwa kiongozi katika usimamizi na uibuaji wa fursa za kichumi na kijamii zinazopatikana kwenye ngazi za msingi na ushirikishaji wa wananchi na wadau wa maendeleo pamoja ukosefu wa maadili ni changamoto nyingine.

Mkuu huyo wa mkoa alikumbusha majukumu ofisa tarafa na utendaji wa kata kuwa ni pamoja na kumwakilisha mkuu wa wilaya katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali kuu kwenye maeneo yao.

Mengine ni kuhamasisha na kuhimiza maendeleo wananchi ili washiriki kwenye shughuli mbalimbali kwenye Tarafa walioko, kuwa kiungo kati ya serika kuu na wananchi katika ngazi ya tarafa, kushughulikia malalamiko ya wananchi na kufuatilia pamoja na kuwahimiza utekelezaji wa sera za serikali katika maeneo yao ya kazi na kuhakikisha kuwa zinatekelzwa ipasavyo.

Alisema pamoja na kushiriki na kutoa ushauri kuhusu upangaji wa mipango ya maendeleo katika maeneo yao, mtendaji mkuu wa kata ni kiungo cha uongozi kwa idara zote ngazi ya kata, kuandaa mpango kazi wa maendeleo ya kata na kuwakilisha kwa mkurugenzi wa halmashauri kupitia kwa ofisa tarafa.



# Adaiwa kuuawa kwa kipigo na mpenziwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ZAINABU Mwangu (50) mkazi wa mtaa wa Misuna, Manispaa ya Singida, anadaiwa kuuawa na mpenzi wake kwa kupigwa na fimbo katika maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amoni Kakwale, amethibitisha kutokea kwa tukio lililotokea juzi katika mtaa wa Misuna, mjini hapa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Misuna, Khamis Lissu, akizungumzia tukio hilo, alisema liitokea juzi usiku wa manane. Alisema mwanamke huyo ambaye ameacha watoto wawili aliuawa na mpenzi wake kwa kumpiga fimbo ambayo ilimjeruhi kichwani, kifuani, tumboni na mkononi.

Alisema taarifa za tukio hilo alizipata baada ya kupigiwa simu na mjumbe wa nyumba kumi (balozi) wa eneo hilo, akimfahamisha kuwa katika mtaa wake kuna tukio na kabla ya kwenda eneo la tukio alimpitia Mkuu wa Polisi wa Kata.

Lissu alisema baada ya kufika nyumbani kwa marehemu akiwa ameongoza na baadhi ya ndugu zake, akiwamo mama yake mzazi, walimkuta Mwangu, maarufu kama Mama Khadija, akiwa amelala sakafuni akiwa hana nguo na mwili wake ukiwa na majeraha sehemu mbalimbali za mwili.

"Tulipomwuliza nini kilichomsibu. Kwa kweli hajitambui kutokana na kipigo na alifanikiwa kutamka neno moja tu, simu," alisema.

Alisema walimchukua kwenda naye katika kituo cha Afya Sokoine akiwa hajiwezi kutokana na maumivu makali aliyokuwa nayo na wakati akiendelea kupatiwa matibabu, alifariki dunia.

**"Tulipomwuliza nini kilichomsibu. Kwa kweli alikuwa hajitambui kutokana na kipigo na alifanikiwa kutamka neno moja tu, simu," alisema.**

Lissu alisema jana asubuhi, baadhi ya majirani akiwamo baba mzazi wa marehemu, walimwona mwanamume aliyekuwa akiishi naye akipiga mswaki nje ya nyumba ya marehemu na walipomuuliza kuhusu hali ya mwenzake (Zainabu) aliwaambia kuwa hajambo.

Naye Mjumbe wa Nyumba Kumi wa Shina Namba 17, Rehema Athuman, alisema walipofika ndani walikuta fimbo ambayo ilikuwa imechanika chanika ikiwa na damu na mwili wa marehemu ukiwa una majeraha ya kama mtu aliyekuwa amekatwa katwa na kitu kama wembe hasa sehemu za tumboni, kifuani na mgongoni.

Baadhi ya wanawake wa mtaa huo wameonesha kusikitishwa mno na kitendo hicho kilichopoteza uhai wa Zainabu ambaye walisema alikuwa akifanya kazi nyumba ya kulala wageni ya Buziluga iliyopo mjini Singida.

Aidha, waliliomba Jeshi la Polisi kufanya msako dhidi ya mtuhumiwa wa mauaji hayo ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yake.

Mwenyekiti wa Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Mkoa wa Singida, Ambwene Kajula, alisema vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na jamii yote kwa ujumla havikubaliki hata kidogo na akatumia nafasi hiyo kulaani kitendo achofanyiwa Mwangu.

# TBA yatoa elimu ujenzi Nanenane

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA) imetumia Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya Nzuguni, Dodoma, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya ujenzi.

Meneja wa TBA Mkoa wa Dodoma, Emanuel Wambura, alisema TBA inashiriki maonesho hayo kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu miradi ya ujenzi inayotekelezwa na wakala huo, hususan katika sekta ya kilimo.

Wambura alisema kuwa TBA inaendelea kushirikiana na wakulima kwa kuwashauri juu ya mbinu bora za ujenzi wa nyumba za makazi na kuboresha miundombinu ya biashara ya mazao ya kilimo.

"Tunaendelea kuwashauri wakulima kuhakikisha wanajenga nyumba zao kwa viwango vya juu, sambamba na kuboresha miundombinu inayochangia ufanisi katika biashara ya mazao ya kilimo," alieleza Wambura.

Pia alisema TBA imesimamia mradi mkubwa wa ujenzi wa vihenge na maghala ya kuhifadhia chakula katika mikoa takribani nane nchini, ambapo mikoa mitatu tayari imemaliza utekelezaji wa mradi huo.

"Mradi huu ni wa muhimu sana kwa wakulima kwani unawasaidia kuhifadhi mazao kama mahindi, ambayo yanapata thamani zaidi kabla ya kupelekwa sokoni," aliongeza.

Sambamba na miradi ya kilimo, TBA pia imetekeleza miradi katika sekta ya mifugo kwa kubuni na kujenga soko la mnada wa mifugo katika mkoa wa Geita.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Sarah Kibonde (kushoto), akitoa ufafanuzi kuhusu majukumu ya ofisi hiyo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu (kulia), wakati wa Maonesho ya Wakulima Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EWURA yataka wenye kero kupaza sauti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa rai kwa wananchi ambao hawaridhishwi na huduma wanazozipata za nishati na maji kuwasilisha malalamiko yao ili kupata haki zao.

Ofisa Huduma kwa wateja wa EWURA Kanda ya Kati, Juma Singano, alisema hayo jana kwenye viwanja vya Maonesho ya wakulima Nanenane Nzuguni jijini hapa.

Alisema mamlaka hiyo hupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali baina ya mtoa huduma na mtumia huduma zote zinazodhibitiwa na EWURA.

"EWURA ina utaratibu maalum wa kupokea na kushughulikia migogoro na malalamiko yanayotokana na huduma zinazodhibitiwa katika sekta za nishati na maji ambapo mteja hujaza fomu kubainisha masuala yanayomtatiza kama ankara za maji au kucheleweshewa kuunganishiwa huduma.

"Utaratibu unamtaka mteja kabla ya kupeleka malalamiko EWURA kwanza ayawasilishe kwa mtoa huduma, kwa mfano kwa Dodoma masuala ya maji mteja atawasilisha DUWASA kabla ya kufikisha suala lake EWURA." alisema.

Singano alisema kwa mteja aliyeomba huduma ya kuunganishiwa maji akishalipia gharama za maunganisho, mamlaka ya maji inapaswa kumpatia huduma ndani ya siku saba.

"Endapo siku hizo zikipita bila maunganisho ya maji kwa mteja, mkataba wa huduma kwa mteja kati ya mamlaka ya maji na mteja unamtaka kulipwa Sh.15,000 kwa siku ya nane na kuanzia siku ya tisa na kuendelea, endapo hilo halikufanyika, mteja anatakiwa kulipwa Sh.5.000," alisema.

Alisema ni muhimu kwa mtumiaji huduma majisafi na usafi wa mazingira kuhakikisha anapata mkataba wa huduma kwa mteja kutoka mamlaka ya maji inayomhudumia ili kujua haki na wajibu wake pamoja na viwango vya ubora wa huduma za maji na usafi wa mazingira.

"Ili anapopata changamoto achukue hatua stahiki ikiwemo kuwasiliana na mamlaka ya maji endapo hataridhika na hatua zilizochukuliwa na mtoa huduma ana haki ya kuwasilisha malalamiko yake EWURA ili yashughulikiwe," alisema.

Aidha, Singano alisema katika maonesho ya Nanenane mwaka huu, zaidi ya wananchi 300 waliotembelea banda la EWURA wamepata elimu ya namna ya kuwasilisha malalamiko yanayotokana na shughuli zote zinazodhibitiwa na EWURA.



# Waandishi vijana wafundwa ushujaa

**Na Mwnadishi Wetu**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA) Zanzibar, kimewataka wanahabari vijana kuwa mashujaa na mabalozi wazuri wa kusaidia upatikanaji wa usawa wa kijinsia kwa maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwaendeleza waandishi wa habari vijana kuandika habari za uchambuzi juu ya wanawake na uongozi nchini.

Alisema katika mafunzo hayo wametoa kipaumbele zaidi kwa waandishi vijana ili kuwaandaa kuwa vijana bora katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa wanawake kushiriki katika uongozi.

"Vijana wa kiume haikuwa bahati mbaya kuwachagua nao kuwa washiriki wa mafunzo haya bali tumefanya hivyo kuwajenga kuwa mashujaa, mabalozi na wanaume wa mabadiliko katika kuhamasisha usawa wa kijinsia kwa jamii," alisema.

Aidha, Dk. Mzuri alisema wamechagua vijana wenye taaluma ikiwamo uandishi wa habari, waandaaji na waongozaji wa filamu ambao watasaidia kuelimisha jamii masuala ya usawa wa kijinsia ili wanawake waweze kushiriki katika vyombo vya maamuzi.

Alisema lengo ni kuona ongezeko kubwa la ushiriki wa wanawake kugombea nafasi za uongozi kupitia mipango kazi itakayoandaliwa na vijana hao ambayo itazingatia uchambuzi wa takwimu na maazimio ya nchi yenye kuridhia ajenda ya dunia ya kufikia usawa wa asilimia 50 kwa 50.

Naye Msanii na balozi wa habari Zanzibar, Mustafa Yussuf, aliwataka baadhi ya wanaume kuondosha dhana potofu kwa wanawake katika uongozi na badala yake kuwasimamia ili kutimiza ndoto zao.

"Tumeona idadi ya wanawake viongozi inaongezeka, na ni waaminifu katika utendaji wao hata katika jamii ukilinganisha na wanaume," alisema Mustafa.

# Mabadiliko teknolojia kilimo yaleta tija

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kukua kwa matumizi ya teknolojia ya kilimo nchini, kumesababisha mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Aliyasema hayo alipotembelea na kukagua bidhaa za kilimo na ufugaji katika Maonesho ya Wakulima ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Dole, Wilaya ya Magharibi "A", Unguja.

Hemed alisema maonesho ya Nanenane yanatoa fursa kwa wananchi kupata taaluma ya kulima na kufuga kwa kutumia mbinu za kisasa ambazo humwezesha mkulima kuvuna mazao mengi kwa muda mfupi.

Pia alisema kilimo, ufugaji na mazingira vina tija kubwa katika maisha ya kila siku hivyo ni vyema wakulima na wafugaji kutumia teknolojia ya kisasa ili kuendana na ushindani katika soko la dunia.

Makamu wa Pili wa Rais alisema Serikali itaendelea kuliboresha eneo la maonesho ya wakulima ili kutoa huduma bora kwa wakulima na wananchi na aliwataka wananchi kutembelea eneo hilo kwa lengo la kujifunza kilimo cha kisasa na chenye tija ndani yake.

**Makamu wa Pili wa Rais alisema Serikali itaendelea kuliboresha eneo la maonesho ya wakulima ili kutoa huduma bora kwa wakulima na wananchi na aliwataka wananchi kutembelea eneo hilo..**

Waziri wa Kilimo, Maliasili na Mifugo wa Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, alisema mwamko wa wafanyabiashara katika maonesho hayo umekuwa mkubwa na kuvuka lengo la wizara la kusajili wajasiriamali 500, alisema jambo hilo limewanyima fursa baadhi yao kushiriki katika maonesho hayo kutokana na wingi wa maombi.

Shamata alisema kutokana na mwamko wa wajasiriamali kujikita kwa wingi katika kilimo na ufugaji, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa ndani hasa mazao ya mboga na kupunguza kuagiza bidhaa hizo nje ya Zanzibar .

Alisema kwa sasa serikali kupitia Wizara ya Kilimo, inajipanga kupanua wigo zaidi wa maonesho hayo kwa kuboresha miundombinu katika maonesho hayo ili kuwawezesha wafanyabiashara kuonesha biashara zao katika mazingira bora yenye kuleta ufanisi wa ufanyaji wa shughuli zao.

Washiriki wa maonesho hayo walisema wamefaidika na huduma ya ikiwamo kupatiwa mikopo ya kujiendeleza kibiashara sambamba na kupatiwa elimu juu ya kilimo na ufugaji wa kisasa wenye tija zaidi.



Wanachama wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Zanzibar, Abdi Mahmoud (wa pili kulia mstari wa mbele), wakiwa katika matembezi kwa kutumia baiskeli, kwa ajili ya kukagua miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wapewa michongo fursa kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kuchangamkia kazi za ujasiriamali ambazo zitawainua kiuchumi kutokana na kuwapo kwa fursa nyingi, ikiwamo mikopo kwa vikundi.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana, Shaibu Ibrahim Ahmed, alisema katika kongamano la vijana kuelekea Siku ya Vijana Duniani ambalo limejikita katika kuibua fursa ziliopo katika Serikali ya Zanzibar katika uchumi wa bluu litakalofanyika Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja.

Ahmed alisema serikali imeweka kipaumbele kwa kundi la vijana wakiwamo wanawake kujikita katika kazi za ujasirimali ambazo ndizo zitakazowainua kiuchumi.

Alisema kupitia fedha za UVIKO-19, serikali imetenga Sh. bilioni 45 kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wa mazao ya baharini kupiga hatua katika mageuzi ya kiuchumi katika kilimo cha mwani, ufugaji samaki na matango bahari.

Kwa mujibu wa Ahmed, wanawake katika uzalishaji wa mazao ya baharini wanayo nafasi ya kutumia mageuzi ya kilimo katika usarifu wa uzalishaji ikiwamo mwani na serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha mwani, Chamanangwe, kisiwani Pemba.

"Wanawake na vijana ni wazalishaji wa mazao ya baharini, hivyo zitumieni fursa zilizopo ikiwamo mikopo ya kujiinua kiuchumi kwa kutumia faida ya viwanda vya kusarifu mazao ya baharini ambavyo viko katika hatua ya mwisho kukamilika," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Fatma Mbarouk, aliwataka wajasiriamali vijana na wanawake kujipanga zaidi na fursa nyingi zinazokuja zikiwamo za ujenzi wa maeneo ya viwanda ambavyo vitazalisha ajira nyingi na kukuza pato la taifa.

Alisema serikali inakamilisha ujenzi wa kiwanda cha usarifu na kuongeza thamani ya Mwani Chamanangwe, Kaskazini Pemba ambacho kitawawezesha wakulima wa Mwani kuzalisha zao hilo kwa kiasi kikubwa ambao kwa asilimia 85 ni wanawake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



REGINA KWANI NI KOSA? Uk.14

JUMAMOSI AGOSTI 10, 2024



# Unamjua DJ Ally B?

KATIKA tamasha la 'Wiki ya Mwananchi' licha ya mashabiki kupata burudani tosha kutoka kwa wasanii mbalimbali wa Bongo Fleva, lakini kivutio kikubwa kilikuwa kwa mburudishaji maarufu, Ally Suleiman Simba, maarufu kama DJ Ally B.

Dj Ally B alionekana kuwapagawisha watu waliohudhuria tamasha hilo kiasi ambacho kiliwafanya wengi wao kushindwa kukaa kwenye viti vyao kwa kucheza ngoma kali pamoja na mtindo wake wa kupiga kelele.

Basi kama wewe ni miongoni mwa watu waliovutiwa na kazi yake, ni muhimu kumjua mwamba huyu wa kuburudisha.

DJ Ally B, amekuwa akitumbuiza katika kumbi na vituo mbalimbali vya redio kwa zaidi ya miaka kumi.

Akiwa amezaliwa mwaka 1986, mkoani Kilimanjaro amekuwa na mafanikio makubwa katika sekta ya burudani na kupendwa na watu wengi.

Mwenyewe anasema kazi hiyo ya muziki aliianza 2002, baada ya kujaribu kazi nyingi na ngumu ambazo zilimpatia usugu wa maisha.

"Mimi sikusoma niliishia darasa la saba, kutokana na sababu kuwa sina elimu nilifanya kazi ngumu ili kujikimu kimaisha, lakini sikufanikiwa, ndipo nikageukia kazi ya kuburudisha muziki," amesema Dj AllyB

Hata hivyo utumbuizaji wake unakuwa tofauti na wa kipekee kutokana na upigaji kelele.

Amewahi kufanya kazi katika klabu za burudani katika majiji makubwa nchini pamoja na sherehe mbalimbali za kijamiii.

BASI SAWA

## Makabila ampa ushauri Mwijaku

MWANAMUZIKI wa Singeli, Dula Makabila, amemshauri mwigizaji na mtangazaji, Mwijaku, kuwa na ukomo wa meneno kutokana na kauli zake wakati mwingine zinamuadhibu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo wa Singeli, amesema kitendo cha kuahidi kumtoa mke wake na kumpa Ali kamwe, endapo timu ya Simba itakapofungwa na Yanga ni kosa kubwa.

Amesema binafsi sijafurahishwa na kauli hiyo, na kumtaka kumuomba radhi mke wake kwa kuwa mwanamke ana thamani kubwa ndani familia na jamii kwa ujumla.



## Afande Sele kuoa tena

MWANAMUZIKI mkongwe, Afande Sele, amesema baada ya kukaa upweke kwa miaka mingi, anatarajia kufunga ndoa kuondokana na hali hiyo.

"Kukaa upweke ni jambo gumu, siku si nyingi nitafunga ndoa ili niondokane na hali hii. Kuna kuumwa na matatizo mengi mwanamke ni muhimu kuwa naye," amesema

Amesema, anashukuru tangu mke wake alipofariki alikabiliana na hali ngumu, lakini alifanikiwa kupita na sasa anataka kuangalia njia mpya ambayo anaamini itampa furaha.





## Ukishangaa ya Lupita...

MWIGIZAJI maarufu kutoka Kenya, Lupita Nyong'o, ameibua mjadala kwa mashabiki zake baada ya kusherehekea miaka mitatu ya kuzaliwa paka wake.

Kupitia Instagram, binti Lupita ambaye ni mshindi wa tuzo za Oscars mwaka 2014, alichapisha picha kadhaa akiwa amemuandalia paka wake sherehe ya kuadhimisha umri huo.

"Nenda Yoyo! Ni siku yako ya kuzaliwa,tafadhali ungana nami katika kumtakia kheri ya miaka mitatu ya kuzaliwa!" ameanmdika huku akiwataka wafuasi wake kumtakia kheri ya kuzaliwa mnyama huyo.



## Diamond avulia kofia Komasava

MSANII maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amesema ngoma yake Komasava, imemfanya kuwa na kiburi kutokana na kuwa kinara kati ya kazi zake zote.

Akizungumza hivi karibuni, Diamond amesema katika miaka 15 ya safari yake ya muziki, ngoma hiyo hakufikiria kama itakuwa kubwa na kuushtua ulimwengu kwa kupendwa na wengi.

"Kama nikisema ukweli, nilijua ngoma hii ni nzito lakini sikuwahi fikiria itakuwa kubwa hivi kwa sababu wakati mwingine unatoka nje ya studio na unajua ngoma hii ni nzuri na watu wataipenda lakini sikudhani itapata ukubwa huo," amesema.

## Walitisha sana, wako wapi?

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 2000 na kuendelea wakati muziki wa dansi ukiwa kwenye chati, mbali na waimbaji, kuliibuka marapa wengi ambao walikuwa wakiweka vionjo kwenye muziki.

Baadhi ya marapa maarufu waliokuwapo ni kama, Ramadhani Masanja maarufu kama Banza Stone, Msafiri Diof, Kalala Junior, Papy Kocha Mtoto wa Mfalme na wengine wengi ambao walisababisha muziki wa dansi kupendwa na kuwa na mashabiki wengi.

Baadhi yao pia ni waimbaji.

Hata hivyo, walikuwapo baadhi ya marapa ambao hawakuwa na majina makubwa, lakini walishiriki kutoa mchango mkubwa kwenye tasnia ya muziki wa dansi.

Marapa ambao waliokuwa hawana majina makubwa kwa sasa wamesahaulika. Hawajulikani walipo kwa mashabiki wa muziki huo, ingawa inawezekana wanapiga muziki hotelini, wameanzisha bendi zao au wanafanyabiashara zingine huku muda wa ziada wakijishughulisha na muziki.

Leo tutawaangalia marapa ambao kwa sasa hawazungumziwi sana, na ni kwa sababu tu hawakuwa na majina makubwa sana kama wenzao, lakini waliitendea haki muziki wa dansi.

**Gyason Semsekwa**

Ni rapa wa zamani wa bendi za Extra Bongo, African Stars 'Twanga Pepeta', na Chipolipolo. Mara ya mwisho alikuwa ameanzisha bendi yake aliyoiita Tamba Stars.

Kabla ya hapo katikati ya miaka ya 2000, alipatwa na matatizo ya uvimbe kwenye koo, lakini alipatiwa matitabu ingawa alikaa kwa muda hadi kurejea tena kwenye masuala ya muziki.

Semsekwa anakumbukwa sana kwa rapu zake zilizokuwa zikiwachizisha mashabiki ukumbini na hata redioni. Rapu hizo ni "Kichaa kapewa rungu usijaribu kupita mbele yake". Nyingine ni 'Usimuige kasuku kuongea." Ni moja kati ya rapu zilizokuwa maarufu sana za rapa huyo ambaye ni kama amesahaulika hivi.

**Mussa Karenga**

Huyu naye ni mmoja wa marapa mahiri ambao hawakujaliwa kupata majina makubwa.

Alikuwa akihudumu kwenye bendi ya 'TOT Plus'. Hakupata ustaa sana kutokana na marapa aliowakuta, lakini kuna kazi kubwa aliziifanya kwenye baadhi ya nyimbo ikiwamo, "Kaona mambo hayawezi."

Alirapu kipande ambacho kilipendwa sana "La Mujer de mi vida eee, erototototo mwanamke wa maisha yangu alee erotooooo."

**Khalid Chokoraa**

Chokoraa ni mmoja wa marapa ambao angalau yeye alipata umaarufu kidogo na hasa alipounda bendi ya 'Mapacha Watatu' na wenzake Kalala Jounior na Jose Mara.

Naye amezunguka bendi kadhaa, akitoa mchango wake. Hivi karibuni alijiingiza kwenye masumbwi, ingawa alikuwa bado hajaacha muziki. Kwa sasa hasikiki sana kama zamani.

**Kalidjo Kitokololo**

Huyu ni rapa wa FM Academia (pichani). Kama humjui, basi ile rapa kali katikati ya miaka ya 2000 iliyokuwa ikiimbwa "Hii ni ajabu ya bata kutingisha bodi manyoya, mgongo tingisha mama, mgongo tingisha..." Huyu ndiye Kadjo Kitokololo. Alitikisa kwa rapa hiyo na nyingine nyingi.

Kwa sasa hasikiki tena, ingawa inawezekana bado yupo kwenye tasnia ya muziki.

**Saulo John 'Ferguson.'**

Ni mmoja wa marapa wa Twanga Pepeta na Mashujaa ambao hawakuwa na majina makubwa sana, lakini walifanya kazi kubwa sana, katikati ya marapa maarufu kama kina Msafiri Diof.

Naye hasikiki sana kwenye ulimwengu wa muziki, ingawa hakuna taarifa kama anaendelea, au yuko wapi kwa sasa.


KHALID CHOKORAA




## Kaniki haina urembo

**Na Adam Fungamwango**

KANIKI ni vazi la khanga lisilo na urembo wowote zaidi ya rangi moja nyeusi iliyokolea sana, na ni miongoni mwa mavazi maarufu kwenye jamii za Kiafrika. Baadhi hulihusisha na mambo ya kishirikina.

Baada ya kupata maana ya vazi hilo, tunakwenda katika filamu yetu ya leo, iitwayo 'Kaniki Nyeusi'.

Baadhi ya wasanii walioicheza ni Faraja Msongela, Grenda Mushi, German Adam, Juma Said na wengineo.

Kwenye kijiji kimoja cha Manoelo ambacho mwenyewe aliyekivumbua au mwanzilishi wa kijiji hicho alitaka kila anayeishi hapo avae nguo aina ya kaniki.

Alikuwa na sababu kwani kuna mzimu ambao huwadhuru wote ambao wanakiuka sharti la kutovaa kaniki.

Hata kizazi kilichofuatia waliendelea kutekeleza mila hiyo. Haikukatazwa kwa mwanakijiji akitoka ndani ya kijiji hicho asivae, ila anapokuwa ndani ni lazima avae. Si mwanaume, mwanamke, kijana wala mzee.

Kuna mlevi mmoja anaitwaye Kagame, yeye alikuwa hataki kabisa kuvaa mavazi hayo. Akavaa anavyojua mwenyewe. Kilichompata, mwenyewe alikubali.

Kuna mama mmoja ambaye alikuwa na binti yake aitwaye Nyendo. Yeye alipata bahati ya kwenda mjini.

Baada ya miaka mingi alirejea akiwa na mchumba wake Fred. Pamoja na kwamba alikaribishwa vizuri, lakini alikumbushwa kuwa baada ya siku moja tu, adumishe mila kwa kuvaa kaniki ili waweze kuwa salama.

Walikataa na kuendelea kuvaa mavazi yao ya mjini. Mama Nyendo aliitwa na Mwenyekiti wa Kijiji na kuambia amuonye binti yake, lakini binti na mpenzi wake walikataa. Waliendelea kuvaa viwalo vya kisasa.

Siku isiyo na jina walikuwa katika matembezi yao ya kawaida, mara gafla Fred alianguka na kuzirai. Hali hiyo ilileta taharuki na kupelekwa kwa mganga ambaye aliwaambia kuwa lazima mila wazidumishe, mgeni huyo na Nyendo kwa kuvaa kaniki.



# Rema kumbe alikomazwa mapema

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Rema, amesema ameathirika katika utendaji wake wa kazi kutokana na vifo vya baba na kaka yake.

Akizungumza na GRM Daily, mwimbaji huyo alieleza kuwa, kutokana na vifo hivyo amejikuta amebadilika na kuwa mtu mzima kutokana na majukumu mengi kumlemea.

"Ninahisi nilikua haraka sana. Maisha yalinigeukia sana nilipofiwa na baba na kaka yangu. Ni kama vile uzito ulivyokuwa mabegani mwangu na ilinilazimu kuuza utoto wangu ili tu kutunza familia," amesema Rema.



## Vybz Kartel bado hali tete

MWANAMUZIKI maarufu wa Jamaica Vybz Kartel, anayejulikana kama  Adidjah Palmer, amesema kwa sasa anaangalia kuhusu afya yake ambayo imeonekana kutetereka akiwa gerezani.

Vybz aliachiliwa huru Julai 31, mwaka huu na saa chache baadaye aliachia Albamu yake mpya ambayo nyimbo zake zinatamba katika majukwaa mbalimbali ya muziki.

"Kiafya sipo vizuri, unajua ninafanyia kazi afya yangu kwa sasa, lakini hisia za kuwa huru ni jambo la kushangaza,"amesema Vybz.

Kartel anapambana na ugonjwa unaofahamika kama autoimmune ambao huathiri tezi na kuathiri ufanyajikazi wa moyo.


## Oxlade kuna na Albam

MKALI wa Afrobeats kutoka Nigeria, Oxlade ametangaza kuachia albamu yake ya kwanza 'Oxlade from Africa' itakayotoka Septemba mwaka huu.

Kupitia video fupi aliyoiweka kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii, mwanamuziki huyo amesema Albamu hiyo itatolewa tarehe 20 Septemba 2024 na itakuwa kama zawadi kwa mashabiki ambao amewaburudisha karibu mwongo mmoja.

Katika Albamu yake hiyo, Oxlade ameimba nyimbo tofautitofauti ambazo anasimulia hadithi za mapenzi, maumivu, furaha, na changamoto anazopitia.





## Regina kwani ni kosa?

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood Regina Daniels, ameonekana kuchukizwa na kitendo cha baadhi ya watu kupeperusha bendera ya Russia katika maandamano yanayoendelea nchini Nigeria.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Regina aliwaambia wafuasi wake kupinga kile kilochotokea kaskazini mwa nchi hiyo kwa waandamanaji hao kupeperusha bendera za kigeni.


"Halo watu wote, mnaona kinachotokea kaskazini? Waone wakipandisha bendera ya Urusi, haya ndiyo tunayoyataka? Kumbuka,  inaweza kukufikia," alisema msanii huyo huku akionekana akiwa na mavazi ya kihafidhina.

## Juju akumbuka alivyopendwa

MWIMBAJI mkongwe kutoka Nigeria, Juju Sunny Ade, amefunguka kuhusu uhusiano wake kimapenzi na  mwanamuziki Onyeka Onwenu, ambaye amefariki dunia.

Hivi majuzi Sunny Ade aliitembelea familia ya Onwenu na baada ya ziara yake, alimwelezea Onwenu, kama mwanamke wa maisha yake na alimfanya kuhisi ana msaidizi mwenye nguvu.

"Siwezi kuelezea, yeye si mwanamke wa kawaida tu, alikuwa mtu ambaye angekaa chini na wewe na alikuwa akihitaji kupata ushauri sahihi kila wakati." amesema.





# DCEA yateketeza magunia 173 ya bangi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Kaskazini, katika harakati za kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, imeteketeza magunia 173 ya bangi na kufungua kesi 36 mahakamani.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa DCEA Kanda ya Kaskazini, Sara Ndaba, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya 30 ya Nanenane yaliyofikia tamati juzi katika viwanja vya Themi, Njiro jijini Arusha.

Aidha aliwataka wakulima wanaojihusisha na kilimo cha dawa za kulevya, zikiwamo aina ya bangi na mirungi kuacha mara moja.

Ofisa huyo alisema kilimo hicho ni haramu na kuna sheria zimetungwa kwa ajili ya kuwakamata wahusika watakaobainika kulima zao hilo, na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

"Katika maonesho haya, tumekuwa tukitoa elimu juu ya athari za bangi au kilimo cha bangi na kumtaka mkulima kuepuka vishawishi vya kupata fedha za haraka na kuingia katika kilimo hicho,tunatoa elimu ili asiweze kuingia katika kilimo cha bangi kwa kuwa ni kinyume na sheria ,"alisema.

**"Katika maonesho haya, tumekuwa tukitoa elimu juu ya athari za bangi au kilimo cha bangi na kumtaka mkulima kuepuka vishawishi vya kupata fedha za haraka...**

Aliwataka wakulima wanaolima mazao ya dawa za kulevya kuacha mara moja badala yake walime mazao ya chakula na biashara, ambayo yanaruhusiwa.

Hadi sasa, alisema wametoa elimu hiyo kwa wananchi wa vijiji vya Kisimiri na Losinoni vilivyopo wilaya ya Arumeru mkoani hapa kwa kuwa ni maeneo yanaongozwa kwa kulima bangi.

"Tulipokuwa tunatoa elimu hii, tulibahatika kwenda na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, na alitoa wito kwa wananchi hao kulima mazao mbadala kama pareto ambalo ndio zao linalostawi vizuri kwenye maeneo hayo," alisema. Pia alisema wakulima hao waliwaeleza sababu ya kulima mazao hayo kuwa ni ukosefu wa maji pamoja na miundombinu ya barabara.

Alisema baada ya kutoa elimu hiyo, walikwenda kufanya tathimini wakiwa na maofisa kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa na kuwaeleza namna gani watachanganua matatizo hayo ikiwamo kupata huduma bora za barabara pamoja na maji.

Kadhalika, alisema katika kuendeleza kutoa elimu mkuu wa wialaya hiyo katika ziara zake za kikazi alizungumza na wananchi hao.

Alisema Kaganda,aliwataka wananchi wa maeneo hayo, kulima mazao mbadala na kuacha mara moja kilimo cha bangi.

# Kero huduma za afya yapatiwa ufumbuzi

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

KUKOSEKANA kwa huduma za afya kwa muda mrefu kwenye machimbo ya madini ya Tanzanite katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, hatimaye ufumbuzi umepatikana baada ya serikali kuweka mpango wa kujenga zahanati ya kisasa.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, alisema ukosefu wa huduma za afya kwenye machimbo hayo,utafikia ukomo mwaka huu baada ya kujengwa kwa zahanati hiyo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa kikao cha kamati iliyoundwa kwa ajili ya eneo tengefu la Mirerani, Lulandala alisema mwaka huu zahanati hiyo itajengwa kwenye machimbo ya madini hayo.

Alisema ujenzi wa zahanati hiyo uamuzi umefikiwa kuwa itajengwa na serikali wakishirikiana na wadau wa maendeleo.

Pia alisema watatekeleza agizo la serikali la kuhakikisha zahanati inajengwa kwenye machimbo ya madini hayo, ili wachimbaji madini na watu wengine wapate huduma za afya.

"Tumeshazungumza juu ya hilo, kuwa wadau wa maendeleo wa eneo hili, watajenga kwa kushirikiana na serikali kama sehemu ya kurudisha walichokipata kuwa huduma kwa jamii," alisema Lulandala.

Hata hivyo alisema pia wamelenga kuhakikisha wanaboresha miundombinu ya barabara kwenye machimbo hayo, ili kutekeleza maelekezo yalitolewa.

"Tutatekeleza maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara,Queen Sendiga, alipofika Mirerani kuhusu uboreshaji wa miundombinu na pia agizo la viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM),walipolitoa kwetu serikali,"aliongeza Lulandala.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Bahati Mushi, alisema hatua ya kujengwa kwa zahanati kwenye machimbo hayo,ni vyema kwa kuwa itawanufaisha wahusika ambao kwa miaka mingi hawakupata huduma za afya.

"Kwa muda mrefu huduma ya afya ilikosekana kwenye machimbo ya madini ya Tanzanite ila kwa hatua hii itakuwa vyema mno tunampongeza DC wetu Lulandala kwa kusimamia hili," alisema.

Mchimbaji wa Madini ya Tanzanite, Michael Mollel, alisema ujenzi wa zahanati machimboni itawasaidia kwa kuwa watapata huduma za afya kwa karibu pindi kukitokea changamoto ya afya.

"Huduma ya afya kwa wachimbaji hivi sasa haipo zaidi ya kuwa na huduma ya kwanza kwenye migodi pindi changamoto ya afya ikitokea kwa hili la zahanati litakuwa bora zaidi," alisema.

Alisema wanatarajia huduma ya zahanati ikipatikana kwenye migodi watakuwa na nafasi nzuri ya kupata matibabu pindi wachimbaji madini wakiugua.



Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Kaskazini, Sara Ndaba (wa tatu kushoto), akitoa maelezo kuhusu shughuli mbalimbali za idara yake kwa wananchi waliotembelea Maonesho ya Wakulima Nanenane, Njiro jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# TARURA kujenga barabara km 177

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani Manyara inatarajia kuanza ujenzi wa barabara kwa umbali wa kilometa 176.9 hivi karibuni.

Katika ujenzi huo wa Barabara kilometa 8.3 zitajengwa kwa kiwango cha lami zikijumuisha madaraja makubwa tisa na madaraja madogo 53 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu hiyo ili kuinua uchumi wa wananchi.

Meneja wa TARURA mkoani hapa, Salim Bwaya, alisema hayo wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.2. Alisema mikataba hiyo wamepatiwa makandarasi wazawa ambapo itasaidia kukuza uchumi wa nchi na kuwaletea wananchi maendeleo.

Alizitaja kazi zitakazofanywa na makandarasi hao kuwa ni matengenezo ya kilometa 142, uboreshaji wa barabara za udongo na kuzibadilisha kuwa za changarawe kwa kilometa 26.6 na ujenzi wa madaraja makubwa tisa, madaraja madogo 53 na kujenga barabara kwa kiwango cha lami kilometa 8.3.

Aidha, alisema Januari 22, mwaka huu, mikataba saba ilitiwa saini kwa mwaka wa fedha uliopita ambayo ilikuwa na thamani ya Sh. bilioni. 2.3.

Meneja huyo alisema kati ya mikataba saba iliyotiwa saini Januari 22, minne imekamilika na mingine mitatu iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na itakamilika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha.

Alitumia fursa hiyo kuwahakikishia makandarasi waliopewa zabuni kuwapa ushirikiano katika kazi zao.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema fedha wanazolipwa ni kodi ya wananchi hivyo iwaume.

Sendiga aliwaagiza makandarasi kuhakikisha wanaonekana maeneo yao ya kazi kila anapopita kufanya ukaguzi awakute na sio kuwatuma mafundi wao tu.

"Sitegemei kusikia mnadaiwa na vibarua au mama lishe na wakuu wa wilaya na mameneja wa wilaya hakikisheni mnatambulisha miradi kwa wananchi maana miradi ni yao," alisema Sendiga.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi wenzake, Anna Sanga, alisema watajitahidi kufanya kazi kwa wakati na viwango kama walivyosaini kwenye mikataba.

Aidha, Sanga aliiomba serikali kuwalipa kwa wakati wanapofanya kazi kwa kuwa makandarasi wazawa wana hali za kawaida.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Nana Njige na Rahma Shally wanawake waliowafungulia njia kina Nandy, Zuchu...



**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka ya hivi karibuni imeonekana kuwa, wanawake ndio wazalishaji mali wakubwa, wamekuwa ndio wafanyabiashra nyingi halali na walipa kodi, na wamekuwa juu kwa kipato cha mtu mmoja mmoja, wakielekea kuwapiga kumbo hata wanaume.

Wanawake kwa sasa wamekuwa wakijishughulisha zaidi tofauti na zamani. Wala si ajabu tena kwa sasa ukaamka saa 10 alfajiri ukaenda kupanda daladala, ukakutana na akinamama wakienda kazini na wengine kwenye biashara zao. Tena ndani ya daladala wanakuwa wengi zaidi alfajiri kuliko wanaume.

Wameondokana na dhana ya kwamba kinamama kazi yao ni kukaa nyumbani na kuletewa na wanaume, kitu ambacho wakati huo kilikuwa kikiwapa umasikini mkubwa na kunyanyasika.

Miaka ya nyuma ukimuona mwanamke anaendesha gari kila mmoja anashangaa. Na ndiyo maana ilikuwa ni ajabu kuona mwanamke ni mwanamuziki.

Wanawake walikuwa na vipaji vya muziki tangu zamani, lakini ni wachache sana, waliobahatika kuingia kwenye fani hiyo, kwani hata wanaume tu walikuwa wakikatazwa na wazazi wao, sembuse mwanamke?

Ilichukuliwa kama si kazi, bali ni burudani na uhuni. Kwa sasa si hivyo tena kwani muziki ni kazi. Hawa wasanii wa kike tunaowaona kwa sasa kina Zuchu, Nandy, Vanessa Mdee na wengine wengi, msingi wao ni wanamuziki wa kike ambao walijitoa muhanga wakati huo, bila ya kujali wataonekana vipi katika jamii, au kutengwa na familia, wakaamua kuingia kwenye fani hiyo.

Tofauti na wazazi wao walivyokuwa wakifikiri. Mathalani, fani hiyo iliwapatia sifa na umaarufu mkubwa, siyo wao tu hata na wazazi na familia zao, kiasi kwamba wameendelea kukumbukwa vizazi na vizazi, tofauti na kama wasingekuwa wanamuziki.

Baadhi ya wanamuziki wa kike nitakaowataja hapa, wasingeandikwa, au kukumbukwa licha ya kwamba baadhi yao wamefariki kama wangeingia kwenye fani zingine au kuolewa tu na kukaa nyumbani. Wasingejulikana na watu wengi na mpaka sasa, na wangeendelea kukumbukwa na watu wachache tu wenye nasabu nao.

Ili kuonyesha kuwa muziki si uhuni, wanamuziki hao wa kike, licha ya kazi hiyo, waliolewa, wakapata watoto na kuendesha familia zao kama mama.

Tabia Mwanjelwa ni mmoja wa wanawake wa mwanzo nchini Tanzania kuvunja minyororo, kwani sauti yake ilianza kusikika miaka ya 1980, akiwa na bendi ya Maquiz Du Zaire, akiimba nyimbo kama 'Maisha ni Safari Ndefu', 'Jane', na zingine. Baadaye alijiunga na bendi ya Orchestra King Kiki Double O, chini ya mwanamuziki Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki, ingawa hakufanikiwa kurekodi. Ni mwanamuziki wa kike ambaye alikuwa akijiamini, huku baadhi wakidhani huenda si Mtanzania. Ndipo alipopata mwenzake, raia wa Zambia Rose Mwape, ambaye alirithi mikoba yake alipokwenda kwa Kiki. Mwape akiwa Maquiz aliimba nyimbo za 'Makumbele' namba mbili, na 'Nabwela miziki ya Zambia'.

Sauti hizi zilisababisha kuibuka kwa kinadada wengine wa Kitanzania, kama Emma Mkelo ambaye baadaye akawa mke wa mwanamuziki Eddy Sheggy na Nana Njige.

Hawa wote wawili waliibukia bendi ya 'Super Rainbow' chini ya Sheggy, wakaimba nyimbo nyingi kama 'Milima ya Kwetu' sehemu ya kwanza na ya pili, 'Vichekesho', na nyingine nyingi.

Bendi iliposambaratika, kila mtu alichukua njia yake, Sheggy alikwenda Vijana Jazz, watoto wa kike nao wakatafuta malisho yao.

Nana Njige yeye alikwenda bendi mbalimbali kama 'Legho Stars', na baadaye akaibukia Magereza Jazz na kuimba nyimbo mbalimbali, lakini wimbo uliompa sifa ni 'Ashura', ambao aliuimba kwa hisia na ustadi mkubwa.

Emma, yeye alikwenda MK Beats wana Tukunyema mpaka chini, kabla ya kwenda Washirika Tanzania Stars na kuimba pamoja na kina Ally Choki, wimbo wa 'Tuilinde Ndoa', ambao una baadhi ya maneno ambayo anaimba Choki akijibizana na Emma 'uliyosema mke wangu, nimeyasikia, lakini kumbuka mwanzo wa ndoa yetu Emma, nilikueleza ushoga sipendelei, ukikaa na shoga zako, mnaacha kusukana nywele, mnaongea mambo ya umbeya.'

Kuna mwanamuziki mwingine wa kike Kida Waziri ambaye alivuma na kudumu kwa kipindi kifupi, akiwa na Vijana Jazz, hasa kwenye vibao vya 'Wifi Zangu'.

Rahma Shally, yeye aliionekana akiimba vizuri kwenye ngoma za asili maarufu cha JWTZ, wakati huo ngoma zote za asili ziliitwa 'Kibisa', lililotokana na kundi kama hilo lililoitwa DDC Kibisa Ngoma Troupe.

Kwa sababu kundi hilo na bendi ya Mwenge Jazz, zote zilimilikiwa na Jeshi la Wananchi, baadhi ya wanamuziki 'walimchomoa' dada huyo kwenye Kibisa na kumleta kwenye bendi.

Hakuwaangusha, akaibuka na nyimbo mbalimbali kali, ukiwamo ule uliompatia umaarufu wa 'Naomba Tuheshimiane'.

Sauti yake ilizifanya bendi nyingi kumnyemelea, Sambulumaa ikafanikiwa kumchukua na alikwenda kuimba wimbo uliokuwa maarufu sana 'Sitaki visa Vyako' na mwingine akiimba na Zahir Ally 'Zamaradi'.

Alikwenda kujiunga na Vijana Jazz na alifanya vema kwenye wimbo wa 'Saddy.'

Waimbaji wa kike, Rahma Shally (wa tatu kutola kushoto), na Nana Njige ( wa tano kutoka kushoto) wakiwa na wanaimbaji wa kiume, Muhidini Gurumo ( wa kwanza kulia) na Marijani Rajab (wa pili kulia) wakiwa kwenye bendi ya Tanzania All Stars, iliyokusanya mastaa wote Tanzania na kuunda kitu kama timu ya taifa, ikarekodi nyimbo nne, zikiwamo 'Kuwajibika', 'Kifo cha Samora' na nyinginezo Katikati ya miaka ya 1980.

HABARI KIMATAIFA

# Uingereza kulinda usalama wa Mtanzania

Na Maulid Mmbaga

BALOZI wa Tanzania nchini Uingereza Mbelwa Kairuki amesema wamezungumza na Wizara ya Mambo ya Nje ya nchini humo na imemhakikishia usalama wa mtanzania aliyedai yuko hatarini kuuawa na hakuna baya lolote litakalotokea.

Nchini Uingereza kumekuwa na machafuko yanayosababishwa na baadhi ya watu wanaotaka wageni kuondolewa, na saa chache baadae kulionekana kipande cha video kilichomuonesha Martina Farrall raia wa Tanzania akiomba msaada akidai kuwa usalama wake uko hatarini baada ya mume wake kupanga kumuua.

Akizungumza jana kupitia video, Balozi Kairuki, alisema maofisa wake wamezungumza na serikali ya Ireland Kaskazini, anakoishi mtanzania huyo pamoja na polisi kuzungumzia suala hilo.

Alisema kwa sasa Martina yuko salama baada ya kuchukuliwa hatua hizo.

"Kama kuna matatizo yoyote yatajitokeza vyombo vya kule vitachukua hatua, na kuna mambo mengine tumeyabaini kwenye uchunguzi lakini kutokana na sheria za ulinzi wa taarifa binafsi za Uingereza sitaweza kuelezea lakini ieleweke kwamba ndugu yetu yuko salama," alisema Balozi Kairuki.

Aliongeza kwa kuwasisitiza watanzania wote wanaoishi Uingereza kuendelea kuheshimu sheria za nchi hiyo pamoja na kijiepusha na vitu vinavyoweza kusababisha kuwaweka kwenye matatizo.

Aidha, alieleza kuwa siku chache zilizopita nchini humo kulikuwa na maandamano yaliyosababisha vurugu, uharibifu wa mali na watu kujeruhiwa, na kutokana na hali hiyo alitoa wito kwa watanzania kuepuka kwenda maeneo yenye msongamano, na kushiriki kwenye maandamano.

Hata hivyo, alisisitiza kwamba pale watakapohisi wako kwenye matatizo wasisite kuwasiliana na ubalozi kwa njia ya barua pepe au mawasiliano ya simu yaliyowekwa kwenye tangazo lililotolewa awali.

"Bado maandamano yanaendelea katika baadhi ya sehemu, tunasisitiza watanzania waendelee kuchukua tahadhari, na hadi sasa hatujapata taarifa za mtanzania yeyote ambaye amedhurika na tunatumaini wote wanaendelea vizuri," alisema Balozi Kairuki.



Uharibifu unaofanywa na wanajeshi wa Israeli katika eneo la Khan Yunis kusini mwa Ukanda wa Gaza.
**PICHA: REUTERS**

# Wanajeshi Ukraine wazidi kuingia Russia

**KYIV,** UKRAINE

SIKU nne baada ya wanajeshi wa Ukraine kuvuka na kuingia eneo la Kursk nchini Russia, Rais wa nchi hiyo Volodymyr Zelensky, amesema kitendo hicho kina lengo la Russia kuhisi matokeo ya uvamizi wake.

"Russia ilileta vita katika ardhi yetu na inapaswa kuhisi kile ilichokifanya", alisema Zelensky katika hotuba yake.

Aliongeza "Waukreni wanajua jinsi ya kufikia malengo yao. Na hatukuchagua kufikia malengo yetu katika vita,"

Russia ilisema wanajeshi 1,000 wa Ukraine, wakisaidiwa na vifaru na magari ya kivita, waliingia katika eneo lake Jumanne asubuhi katika kile kinachoonekana kuwa moja ya mashambulio makubwa zaidi kufanyika katika ardhi ya Russia tangu vita hiyo kuanza.

Rais wa Russia Vladimir Putin hapo awali aliishutumu Ukraine kwa kufanya uchokozi.

Hadi sasa maofisa wa Ukraine wamekuwa kimya kuhusu mashambulizi hayo.

Hata hivyo, ni vigumu kuelewa hali halisi katika uwanja wa vita na kuna maelezo machache yametolewa kutoka kila upande.

Katika hatua nyingine, jeshi la Ukraine lilisema kuwa limeshambulia uwanja wa ndege wa kijeshi ndani ya Russia na kuharibu maghala kwa kulipua mabomu.

Katika taarifa yake, liliripoti kuwepo kwa moto baada ya kuharibu vilipuzi vingi katika uwanja wa ndege wa Lipetsk, ulioko zaidi ya kilomita 350 kutoka mpaka wa Ukraine.

Viongozi wa mkoa wa Lipetsk walisema wametangaza hali ya hatari katika eneo hilo, na kuthibitisha kuharibiwa kwa kituo cha nishati".

Wakazi wa vijiji vinne vya karibu walikuwa wakihamishwa.

Ripoti zinaonyesha kuwa wanajeshi wa Ukraine wanafanya kazi takriban kilomita 10 ndani ya ardhi ya Russia, hatua inayoelezwa ni kubwa zaidi ya kuvuka mpaka iliyofanywa tangu ulipoanza uvamizi kamili mnamo Februari 2022.

**BBC.**



Wanaanga wa NASA Butch Wilmore na Sunita Williams walichukuliwa kabla ya kuondoka kwenda angani Juni mwaka jana.

# Wanaanga wakwama angani

**WASHINGTON,** MAREKANI

WANAANGA wawili kutoka Shirika la Anga la Marekani, (NASA) wataendelea kubaki angani mpaka mwakani baada ya kushindwa jaribio la kurudi duniani.

Taarifa iliyotolewa na Nasa jana, ilisema wanaanga hao, Barry 'Butch' Wilmore (61) na Sunita Williams (58), waliondoka duniani Juni 5, mwaka huu kuelekea katika Kituo cha Kimataifa cha Anga za Juu (ISS).

Hata hivyo, kwenye safari yao ya majaribio walitakiwa kurejea Duniani ndani ya siku chache, lakini mambo yalikwenda tofauti na ilivyopangwa.

Takriban miezi miwili baada ya kuondoka, wanaanga bado wanaelea angani juu ya Dunia.

Wanaanga hao watalazimika kusherehekea Krismasi na Mwaka Mpya wakiwa angani, hadi hapo utaratibu wa kurudi utakapoandaliwa.

Wilmore na Williams walielekea Kituo cha kimataifa cha anga za juu (ISS) wakitumia chombo cha anga za juu cha Starliner kilichotengenezwa na kampuni ya Marekani ya Boeing.

Kama safari ya kwanza ya ndege ya Starliner, wanaanga hao wawili walipewa jukumu la kupima ufanyaji kazi wa chombo hicho kipya kabla ya kuanza kutumika mara kwa mara.

NASA ilieleza katika kikao na wanahabari kwamba kwa sasa haijulikani ni hatua gani itachukuliwa kuhusu wanaanga hao na chombo chao.

**BBC**

# Kamala, Trump kushiriki mdahalo wa kwanza leo

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAGOMBEA wa urais Marekani, Kamala Harris na Donald Trump, watapambana katika mdahalo wao wa kwanza utakaofanyika leo.

Shirika habari la ABC News, lilithibitisha kuwa litaandaa mdahalo huo.

Kupitia ukurasa wa X, shirika hilo lilisema mdahalo huo upo kama ulivyopangwa. Hivi karibuni Trump alisema atakuwa tayari kufanya mdahalo na mpinzani wake wa chama cha Democratic mara nyingi kabla ya uchaguzi wa Novemba.

"Tunafikiri tunapaswa kufanya midahalo mitatu," Trump alisema, akipendekeza midahalo miwili ya ziada ambayo alisema itaandaliwa na Fox News na NBC.

Harris alithibitisha kwamba atahudhuria mdahalo wa ABC akiwa kwenye hafla katika jimbo la Michigan siku ya Alhamisi.

**BBC**

# Mawazo, fikra za Mwalimu Nyerere zilivyoenea China

**Na Li Chunguang Li Hongfeng**

KWA Chuo cha Afrika katika Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Beijin, Julius Kambarage Nyerere si tu Baba wa Taifa kwa wananchi wa Tanzania, bali pia aliheshimiwa kuwa ni "mwalimu" wao wa kifikra.

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema: "Nchi isiyokuwa na utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu wasiokuwa na roho inayowafanya kuwa taifa."

Akiwa mwanzilishi wa chama tawala cha Tanzania - Chama Cha Mapinduzi CCM na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Nyerere alisukuma mbele harakati za ukombozi wa taifa la Tanzania na kuhimiza mapambano ya kujipatia uhuru ya nchi za Kusini mwa Afrika

Pia mawazo yake kuhusu muundo wa taifa, Umoja wa Afrika na mambo mengine, yamejenga moyo wa "Uhuru" wa Tanzania ulio wa kujitawala na kujiamulia, na Fikra ya Umajumui wa Afrika (Pan-Africanism) ya nchi za Afrika kushirikiana na kujiendeleza.


Kama vilivyoenea barani Afrika kwa Fikra, Mao Zedong na mawazo ya Xi Jinping, utetezi wa kisiasa na mawazo ya utamaduni ya Mwalimu Nyerere pia yameenea sana China katika nusu karne iliyopita.

Mwanzoni, tafsiri za mawazo ya Mwalimu Nyerere zaidi yalikuwa kuhusu wasifu wake, ambao ulienea kupitia vyombo muhimu vya habari vya China na kuwawezesha watu wa taifa hilo kumjua zaidi Rais Nyerere wa Tanzania.


Kuanzia mwaka 1965, kadiri Rais Nyerere alivyofanya ziara nchini China mara kwa mara na kuongeza urafiki kati yake na Mwenyekiti Mao na viongozi wengine, ndivyo tasnifu kuhusu mawazo yake ya utawala wa nchi, maoni na mapendekezo ya sera na hotuba zake zilikuwa zimeanza kutafsiriwa na kuchapishwa kwenye majarida maarufu ya Kichina, kama vile Asia Magharibi na Afrika na Sayansi ya Jamii ya Ng'ambo.

Tasnifu hizo ziliongeza zaidi ufahamu wa watu wa China juu ya mawazo ya Mwalimu Nyerere. Mwaka 1975, kitabu cha Nyerere ambacho ni cha kwanza kinachoeleza maisha ya Mwalimu Nyerere, kilichapishwa na Shirika la Uchapishaji la Umma la Shanghai, kimekuwa njia muhimu kwa wasomaji wa China kumjua zaidi Rais Nyerere.

Kuanzia miaka ya 1980 hadi 1990, ushirikiano kati ya China na Tanzania uliendelea kupanuka katika maeneo ya pande mbili na ya pande nyingi, makala na tasnifu za aina mbalimbali kuhusu mawazo muhimu ya Rais Nyerere na hotuba zake nyingi kuhusu ujenzi wa ujamaa zilitafsiriwa na kuenea nchini China, kama vile kitabu cha Ujamaa - Usoshalisti wa Afrika, ambacho ni kitabu muhimu kuhusu mawazo ya Nyerere kinachojulikana sana kwa wasomaji wa China.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. **PICHA: MAKTABA**




Kitabu kinachoelezea falsafa za Mwalimu Nyerere nchini China.

Oktoba 14, 1999, Mwalimu Nyerere alifariki dunia. Lakini mawazo na siasa yake ambayo ni mali ya urithi yanaendelea kuelekeza maendeleo ya Tanzania na kuhimiza uhusiano wa China na Tanzania uendelezwe siku hadi siku.

Mwaka 2009, kutokana na serikali ya Tanzania kutangaza "Siku ya Nyerere", mashirika ya diplomasia, elimu na utamaduni ya nchi hizi mbili zilianza kufanya utafiti zaidi juu ya mawazo na moyo wa Mwalimu Nyerere kwa kupitia shughuli za majadiliano na utafiti wa taaluma kuhusu mada ya "Siku ya Nyererea nchini China" na maonesho ya utamaduni, zikilenga kufundishana katika mawasiliano kati ya nchi mbili katika sekta ya utamaduni.

Mnamo mwaka 2014, vitabu vya juzuu nne vya filosofia vya Maandishi Yaliyoteuliwa ya Nyerere vilichapishwa nchini China. Mwaka 2022, Wasifu wa Nyerere: Utafiti wa Viongozi wa Afrika wa Muktadha wa Tamaduni Tofauti pia kilichapishwa, ambacho kimekuwa dirisha muhimu kwa Wachina kuelewa mawazo ya Julius Nyerere.

Mwalimu Nyerere hayupo tena lakini mawazo yake yamewasha mwenge juu ya Mlima Kilimanjaro, ambao umekuwa ukiangaza sehemu zote nchini Tanzania na nje ya nchi hiyo.

Mawazo ya Nyerere si kama tu yanaeneza upendo, urafiki, heshima, na matumaini duniani, bali pia yanasukuma mbele maendeleo endelevu ya uhusiano wa wenzi wa ushirikiano wa kimkakati wa pande zote kati ya China na Tanzania.

***(Watafsiri: Chen Lianying Wei na Yuanyuan Yu Minghong)***

## REA yahamasisha matumizi nishati safi kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy, amehimiza wananchi kutumia Nishati Safi ya Kupikia ili kuokoa gharama na muda, kulinda mazingira na afya zao.

Amesema nishati hiyo ni muhimu kwa kuwa teknolojia sasa imeboreshwa na gharama yake ni nafuu ikilinganishwa na nishati zingine.

Mhandisi Saidy alisema hayo juzi mbele ya wananchi waliotembelea banda la REA katika Maonesho ya Siku Kuu ya Wakulima (Nanenane), Nzuguni Jijini Dodoma.

"Tunaendelea kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia kwani ni salama, rafiki na gharama yake ni nafuu kwa kuwa teknolojia sasa imeboreshwa," alisema.

Mhandisi Saidy pia alisema kuna dhana ambayo imejengeka katika jamii kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia ni ghali na si salama na pia chakula kinachopikwa kutokana na nishati hiyo hakina ladha suala ambalo alisisitiza kuwa halina kweli.

"Ninawathibitishia nishati safi ya kupikia ni salama kuliko nishati zingine tulizozizoea. Niwatoe wasiwasi katika hili na tunaendelea kutoa elimu kuhusu usalama na umuhimu wa nishati hii bora," alisema.

Akizungumzia upatikanaji wa nishati hiyo, alisema serikali imetoa ruzuku katika usambazaji wa mitungi ya gesi (LPG) na majiko banifu ili kuvutia wawekezaji wengi na pia kumwezesha kila mwananchi kumudu gharama zake.

"Serikali imekuja na mfumo wa kumrahisishia kila mwananchi hususani yule mwenye kipato cha chini kumudu gharama ya nishati safi ya kupikia kokote aliko ili aachane na matumizi ya nishati nyingine," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameipatia REA jukumu la kuhakikisha inasimamia vyema utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034 ili kufikia 2034 asilimia 80 ya wananchi wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kutuamini na kutupatia jukumu hilo kubwa na tayari kwa kushirikiana na wadau tumeanza utekelezaji wake na tunakwenda vizuri," alifafanua.

Alisema hatua inayoendelea sasa ni kuibua na kuwawezesha wazalishaji wengi wa vifaa vya Nnshati safi ya kupikia ili kuongeza umahiri sambamba na kuwawezesha kutengeneza bidhaa nyingi kwa gharama nafuu na kwa ubora wa kimataifa.

Kwa kufanya hivyo, alisema kutakuwa na ongezeko la matumizi ya nishati safi ya kupikia, ongezeko la ajira na hatimaye kukua kwa uchumi.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

## Damu ya Mariamu-**25**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




"Nimekuita hapa ili nikupe mrejesho wa kile ambacho tumekifanyia kazi mimi na wewe." Afande Willy aliulinza kile ambacho kimewaleta pale. "Nakumbuka kwanza nilihitaji namba za simu ambazo zilitumika kukutumia meseji za vitisho wewe na mpenzi wako ambazo uliniambia hata ukijifanya kama unataka kuwatumia pesa, haitoi majina ya watu, nikwambia namba haipo." "Ni kweli afande."

"Niliifanyia kazi na nikakwambia namba hizo nne, zilisajiliwa na wakala Shida Mrosso pale Tabata, ukaenda kuzifanyia kazi." "Ndiyo." "Unaniletea majina ya Uledi Mwinyimvua alisajili laini mbili za makampuni tofauti na Abbas Abdallah naye alisajili mbili pia." "Ni kweli afande." "Sasa uliponipa niliendelea kufanyia kazi suala hili. Kama nilivyokwambia nafaifanya bila kibali kutoka Jeshi la Polisi, ila kwa ajili ya kukusaidia kama raia mwema, rafiki wa kaka yangu, na pia ikibainika hiki kitu kinaweza kunipa sifa kubwa, ingawa nimejiingiza kwenye hatari kutoka kwa wenzangu ambao ni wala rushwa. Lakini sijali hilo. Nilikwenda kuwakamata hao wote wawili kila mmoja wa wakati wake. Wote wakaniambia wametumwa na mtu mmoja anayeitwa Kalisa Mohamed." Akanyamaza na kumtazama Kamal alivyokuwa anashangaa. "Unamfahamu?" "Hapana simfahamu. Labda nikimuona kwa macho." "Okay, kama askari nikambana, akakubali kuwa ni kweli aliwatuma watu wale waende wakasajili laini hizo, lakini na yeye alitumwa na rafiki yake mkubwa, anaitwa Boniphace Materu." Alipotamka jina lile Kamal alishtuka na macho yalimtoka pima, kiasi cha kuwashangaza na kuwashtua afande Willy na Dokta Shija. Ilionekana kabisa moja kwa moja anamfahamu sana mtu huyo. "Vipi Kamal, mbona umeshtuka?" Afande Willy akauliza. Kamal hakujibu. Alionekana kuendelea kuwaza kama vile anakumbuka kitu fulani. Tayari afande alishaanza kuhisi kuna kitu ambacho Kamal anakifanhamu na kinaweza kabisa kikawa kinakaribia kumaliza utata wao na nani aliye nyuma ya mpango ule wote. Kamal akashusha pumzi nzito. "Ama kweli katika dunia hii, kikulacho ki nguoni mwako."

Kwa jinsi alivyoeleza tu, afande Willy alijua tayari huenda muuaji wa kweli amepatikana. "Unamfahamu vipi mtu huyu?" Dokta Shija naye alimsaidia mdogo wake kuuliza. "Ndiyo, namfahamu. Ni bosi wangu."

"Si ndiyo huyu huyu ambaye ana mpango wa kugombea ubunge?" Akauliza Dokta. "Ndiyo. Mimi nafanya kazi kwenye gereji yake iliyopo Buguruni na mimi amenipandisha cheo kuwa ndiyo msimamizi. Sasa sielewi, kwa nini alipandisha cheo, wakati kumbe ananifanyia hivi!"

"Kamal, ni hivi, huyu bosi wako ndiye aliye nyuma ya mpango huu, na siyo kama amemuua yeye kwa mkono wake, ila ametuma watu ili kumuua mpenzi wako. Huyu ndiye inaonekana alikuwa anamtaka kimapenzi na alikuwa anamkatalia. Sasa kwa sababu asijulikane ndiyo akatengeza mpango wa kukutisha kwa meseji alizotuma zisajiliwe na watu wengine ili asijulikane.

Alianza kumtongoza mpenzi wako, baada ya kukataliwa ndipo alipoanza vitisho kwako na kwake. Kilichomponza mpenzi wako ni kwamba alimjibu kuwa hata kama ukimuua Kamal, hutoweza kunipata kwa sababu na mimi nitajiua."

Maneno hayo yanamkumbusha meseji ya Mariamu aliyoahi kuiona na ndipo alipoamini kuwa alikuwa anampenda sana. Hakujua kuwa meseji hizo zilikuwa zinatumwa na bosi wake, Materu.

"Mtoto wa watu hana kosa, unataka kumuua kwa sababu gani, kwa sababu ya pesa zako, utajiri wako, kumbuka ukifanya hivyo tu, nakwenda kukuripoti polisi, halafu na mimi najiua. Siwezi kuona mtoto wa watu ameuawa kwa sababu yangu, halafu mimi nikaendelea kula raha duniani. Kama huko kuna kuoana, basi tukakwenda kuoana paradiso."

Kitu kilichomshangaza Kamal ni kuona Mariamu alikuwa anajua kuwa meseji ili ilitumwa na Materu. pamoja na kwamba haikuwa namba yake halisi, bali ya kusajili kimagumashi, lakini akaweza kuitambua kuwa ni nani aliyemtumia meseji ile.

Hiyo ilimfanya ajue kuwa Mariamu alikuwa anatongozwa na nani, na ilianza siku nyingi ila alikuwa anakataa.

**Unaniletea majina ya Uledi Mwinyimvua alisajili laini mbili za makampuni tofauti na Abbas Abdallah naye alisajili mbili pia." "Ni kweli afande."**

Kingine ni jinsi mpenzi wake huyo kuweka siri na kutotaka kumwambia kuwa bosi wake Materu ndiye anayemtongoza.

"Nadhani aliogopa kuwa naweza kuacha kazi. Au mimi mwenyewe kufukuzwa kazi, ndiyo maana akakaa kimya na kuwa na siri yake moyoni kwa mtu anayemsumbua." "Kamal, Mariamu amekufa kwa ajili yako. Angemkubalia angekuwa hai mpaka leo hii na nadhani wewe mwenyewe usingejua kama bosi wako anakuchukulia mwanamke." Dokta Shija akadakia. "Hapana Dokta, Materu alitaka kumchukua moja kwa moja, yaani mimi nikuache, sina hadhi ya kuwa naye, hicho ndicho kilichokuwepo."

"Sawa sasa tumejua kuwa tajiri Boniphace Materu ndiye kinara wa mauaji haya. Na yeye ndiye baada ya kufanikisha kutuma watu kumuua Mariamu akahonga baadhi ya madaktari kubadilisha uchunguzi wa kifo kwa sababu ya kuficha ushahidi, baada ya nguvu ya umma pamoja na wanandugu, uchunguzi wa kweli ukafanyika, lakini akabambikiwa muuaji ambaye siye, naye ni wewe. Sasa kinachotakiwa hapa ni jinsi gani ya kufanya ili umma ujue kuwa Materu ndiye kinara wa mauaji." "Ni kweli afande kwa sababu mpaka sasa mimi ndiye natambulika kama muuaji."

"Kaka Shija, kuna nyaraka fulani ambazo zitakuwepo ofisini kwako, nazitaka kwa ajili ya ushahidi, nitakwambia ni za aina gani. Halafu kuna zingine zitakuwa ndani ya ofisi ya Materu. Tukizipata hizi tu, basi tutawabadilisha watu wote na kumuanisha hadharani aliyesababisha mauaji ya Mariamu, lakini tukifanya pupa haitowezekana. Sisi wenyewe tutajua kuwa yeye ndiye aliyeinjinia mauaji kwa sababu za kimapenzi, lakini kuwaaminisha watu kuwa tajiri yule ndiye muuaji na si wewe ni kazi ngumu, pia hata mahakamani utahitajika ushahidi usio na shaka hata kidogo." Afande Willy akatanabaisha. Willy na kaka yake dokta Shija wakapeana majukumu na kumtaka Kamal atulie, kwani kuna kazi moja kubwa atapewa ili kukamilisha ushahidi wa kumtia hatiani Materu, ambaye ni mfanyabiashara maarufu nchini, mwenye makampuni, maduka, gereji, na vitega uchumi mbalimbali nchini, lakini pia akiwa na mpango wa kuwania ubunge katika moja ya majimbo nchini.

"Nakuomba pia, nenda kachukua nguo zako na vitu vyako huko unakuishi, kwa siku hizi chache kabla ya kazi hiyo utakaa hapa." Afande Willy alimwambia Kamal, ambaye aliafiki.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERIKALI YAKOSHWA VIWANGO SIMBA, YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amesema Wizara hiyo imekoshwa na uwezo na viwango vya klabu za Simba na Yanga walivyovionyesha katika mchezo wa nusu fainali wa Ngao ya jamii uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Msigwa alisema, licha ya kuwa Yanga wamefanikiwa kutinga hatua ya fainali, lakini pia Simba wameweza kuonesha kiwango kikubwa.

**"Nazipongeza timu hizi zimeonesha uwezo mkubwa katika mchezo huu ambao ulikuwa na upinzani mkubwa, kila timu imefanya usajili mzuri ambao utaleta mafanikio katika mashindano ya Kimataifa," alisema Msigwa.**

Aidha, Katibu huyo aliupongeza zaidi uongozi wa Simba kwa kuweza kubadilisha kikosi chao kutokana na usajili walioufanya kwa kuchukua wachezaji wenye viwango vya hali ya juu.

Alisema Yanga nayo imezidi kuonyesha ubora wake kwa kuongeza baadhi ya nyota ambao wameonyesha uwezo mkubwa katika mchezo huo, na anaamini timu hizo zitaanza vizuri katika michezo yao ya Kimataifa.

Aidha, alisema mchezo wa fainali utakaozikutanisha Yanga na Azam kesho Jumapili utakuwa mzuri na wenye ushindani kutokana na aina ya timu zinazokwenda kukutana.

"Lakini nitumie fursa hii kuzitakia kila la heri timu zote ambazo zinajiandaa kushiriki mashindano ya Kimataifa, tunaamini zitaenda kupambana na kuendelea kulitangaza taifa," alisema Msigwa.

Yanga na Azam zimetinga hatua ya fainali baada ya Yanga kuichapa Simba bao 1-0 jijini Dar es Salaam, huku Azam FC ikiivurumisha Coastal Union mabao 5-2 katika mchezo ambao ulichezwa Visiwani Zanzibar.

## *Ouma alia na umakini mdogo Coastal Union*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Coastal Union, David Ouma, amesema umakini mdogo wa wachezaji wake uliwagharimu kwenye mchezo wao wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC.

Kocha huyo alisema mabao yote waliyofungwa juzi yalitokana na makosa ya wachezaji wake amabo hawakuwa makini kwenye kujilinda.

Alisema wapinzani wao walitumia mbinu za haraka katika kufanya mashambulizi pale walipokuwa na mpira lakini wachezaji wake hawakuwa makini kwenye kujilinda.

Alisema mbinu hiyo ilifanikiwa kwa wapinzani wao kutokana na wachezaji wake hawakuwa na kasi kwenye kuzuia.

"Tumeadhibiwa kutokana na makosa yetu, wachezaji wangu hawakuwa makini kwenye kujilinda na kuzima mashambulizi ya wapinzani wetu, nimekubali matokeo naenda kufanyia kazi makosa haya," alisema Ouma.

Alisema mara nyingi timu hizo mbili zinapokutana mchezo unakuwa mgumu na kila mmoja anakuja na mbinu ya kutaka kushinda.

"Haikuwa katika mpango wetu kupoteza huu mchezo, tulifanya matayarisho ya kutosha ili kuona hatupotezi ingawa tunajua tunacheza na timu yenye uwezo, lakini wapinzani wetu walituzidi, tunaenda kufanyia kazi mapungufu haya niliyoyaona," alisema Ouma.




Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa kikapu katika uwanja wa kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Dabo: Bado tuna makosa mengi

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kushinda mabao 5-2 katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii juzi kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar dhidi ya Coastal Union, Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema kikosi chake bado kina makosa mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi, vinginevyo yanaweza kuwagharimu mbele ya safari.

Azam ambayo imetinga hatua ya fainali, inatarajiwa kucheza dhidi ya Yanga kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Dabo, raia wa Senegal, alisema licha ya ushindi mnono, lakini hajafurahia kwa jinsi timu yake ilivyocheza hasa kipindi cha kwanza, akionya kuwa inabidi wawe makini sana wanapokwenda kucheza mechi ya fainali dhidi ya Yanga.

"Ilikuwa mechi nzuri, kuna wakati tulicheza vizuri, lakini kuna wakati hatukucheza vyema, tunatakiwa tuwe makini zaidi ya hapa, tumefanya makosa mengi sana hasa kipindi cha kwanza, lazima tuyafanyie kazi mapema yasitugharimu mbele ya safari," alisema Dabo.

Hata hivyo alisema yeye ni kocha, hivyo ana wajibu wa kukaa na wachezaji wake ili kuondoa makosa yaliyojitokeza kwenye mchezo dhidi ya Coastal Union.

"Tulikuwa tukipoteza mipira mingi sana na kujisahau kwenye kukaba, makosa haya tukikutana na timu bora zaidi yatatugharimu, mara moja nayafanyia kazi," alisema.

Katika mchezo huo wa juzi, mabao ya Azam Fc yalifungwa na Jhonier Blanco, Ever Meza, Feisal Salum, Adam Adam na Gibril Sillah.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FELIX ATAKIWA ASTON VILLA

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anataka kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, 24, ambaye ana nia ya kuondoka Atletico Madrid. ***(BirminghamLive),***

### YAMGANDA GORDON

LIVERPOOL inaendelea kumtaka mshambuliaji wa Newcastle United, Anthony Gordon, 23. Mpango wa kumnunua mchezaji huyo ulishindikana mwezi Juni, huenda bei yake ikapanda. ***(Liverpool Echo)***

### ACHEAMPONG AWINDWA

REAL Madrid na Paris St-Germain zinamtazama mlinzi wa Chelsea, Josh Acheampong mwenye umri wa miaka 18, kama chaguo linalowezekana la beki wa kulia. Mwingereza huyo ni mhitimu wa akademi ya Chelsea. ***(Independent)***

### AKARIBIA KUTUA AL AHLI

MLINZi wa West Ham, Kurt Zouma anatarajiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Shabab Al Ahli baada ya kuafikia makubaliano na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

### BUONANOTTE KWA MIKOPO

LEICESTER City inakaribia kumnunua kiungo wa kati wa Argentina na Brighton mwenye umri wa miaka 19, Facundo Buonanotte kwa mkopo. ***(Mail)***

### ZUBIMENDI AOMBWA KUBAKI

REAL Sociedad inajaribu kumshawishi mchezaji anayewaniwa na Liverpool, Martin Zubimendi kukataa kuhamia Anfield. Kiungo huyo wa kati wa Hispania ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 51. ***(Times)***

### LIVERPOOL YAMZUIA SEPP

LIVERPOOL imekataa ofa nyingi kwa mlinzi wa Uholanzi, Sepp van den Berg mwenye umri wa miaka 22. Hoffenheim, Stuttgart, Wolfsburg, Mainz, Borussia Monchengladbach na Bayer Leverkusen zote zinavutiwa nae. ***(Sky Germany)***

### CAJUSTE HUYO BRENTFORD

KLABU ya Brentford imekubali mkataba wa mkopo, na kipengele cha kumnunua ambacho kinaweza kuwa cha lazima cha thamani ya karibu pauni milioni 10 ili kumsaijili kiungo wa kati wa Sweden Jens Cajuste mwenye umri wa miaka 24, kutoka Napoli. ***(Fabrizio Romano)***


### GALLAGHER ANGEACHWA

MKURUGENZI wa michezo wa klabu ya Valencia, Miguel Angel Corona amesema Atletico Madrid ilijaribu kufuta uhamisho wa kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24 ili kutoa kipaumbele kwa kiungo wa kati wa klabu hiyo, Javi Guerra mwenye umri wa miaka 21. ***(Athletic)***

### JAMES SAFI BIRMINGHAM

KLABU ya Birmingham City imekubali mkataba na Rennes kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Wales, Jordan James, 20. ***(Independent)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# JULIAN ARAUJO KUONDOKA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

MCHEZAJI wa kimataifa wa Mexico mzaliwa wa Marekani, Julian Araujo anakaribia kuhama kutoka Barcelona kwenda klabu ya Ligi Kuu ya England Bournemouth, kwa mujibu wa ESPN.

## ●●● Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo amethibitisha huku AC Milan na Real...

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameambiwa hawezi kupata nafasi katika kikosi cha kwanza cha Barcelona kwa msimu ujao na aliarifiwa kwamba watatafuta uhamisho kabla ya kumalizika kwa dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

**Barcelona wako tayari kukubali pendekezo la Euro milioni 10 ikijumuisha euro milioni 7 ambazo hazibadiliki na euro milioni 3 nyongeza.**

Miamba hao wa LaLiga pia wanataka kumhakikishia asilimia ya uhamisho wa Araujo kutoka Bournemouth.

Kifungu kinachowezekana cha kumnunua, ambacho kwa sasa si kipaumbele, kinaweza kujumuishwa.

Kumhamisha Araujo kutamaanisha kuimarika kwa uchumi na unafuu mdogo kwenye njia ya usawa wa kifedha kwa Barcelona.

Araujo pia aliripotiwa kuwa kwenye rada za Sevilla ambayo sasa inaongozwa na kocha wa zamani wa Las Palmas, Francisco Garcia Pimienta, ingawa kuna uwezekano kwamba hawatakuwa tayari kulipa kiasi ambacho Barcelona wanakihitaji. Uhusiano kati ya timu zote mbili pia ni mbaya.

Baada ya kusajiliwa na Barcelona kwa euro milioni tano kutoka LA Galaxy mwaka 2023, Araujo alicheza mechi 25 kwa mkopo akiwa na Las Palmas msimu uliopita.

Beki huyo wa pembeni alirejea Barcelona kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya na akacheza kwa dakika chache kama winga katika mechi ya kirafiki dhidi ya Manchester City.

Hata hivyo, alibaki kwenye benchi chini ya kocha mpya, Hansi Flick katika mechi mbili zilizopita dhidi ya Real Madrid na AC Milan.



# TEN HAG ALIA NA MAJERUHI UNITED IKIIVAA MAN CITY NGAO YA JAMII

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag alisema hatachukua tahadhari na wachezaji wake katika pambano la Leo Jumamosi la Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City licha ya uwezekano wa kubakiwa na mabeki watatu pekee walio fiti kwenye mechi hiyo.

Leny Yoro na Tyrell Malacia tayari wameondolewa na Ten Hag alithibitisha katika mkutano na waandishi wa habari siku ya Alhamisi kwamba kuna "alama za maswali" juu ya upatikanaji wa Harry Maguire, Victor Lindelöf, Luke Shaw na Aaron Wan-Bissaka.

Inawaacha tu Jonny Evans, Lisandro Martínez na Diogo Dalot kama mabeki wakubwa pekee walio fiti kikamilifu, pamoja na beki wa kushoto mwenye umri wa miaka 17, Harry Amass, ambaye alianza katika kichapo cha mechi ya kirafiki dhidi ya Liverpool huko South Carolina Jumamosi iliyopita.

Martínez na Dalot wamerejea tu mazoezini baada ya kucheza michuano ya kimataifa msimu wa majira ya joto na Ten Hag alisema hatawahatarisha wachezaji hao katika uwanja wa Wembley kabla ya mechi ya kwanza ya Ligi Kuu dhidi ya Fulham wiki ijayo.

"Siku zote tunataka kushinda, pia katika mechi zote za kirafiki, ni kuhusu kombe, na tutaiweka nje timu ambayo ina ushindani mkubwa kushinda kombe hili," alisema Ten Hag.

Martínez na Dalot wote walikosa ziara ya Marekani baada ya kushiriki katika Copa América na Ubingwa wa Ulaya.

Bruno Fernandes na Alejandro Garnacho pia ni sehemu ya kundi la wachezaji wa kimataifa ambao wamerejea mazoezini Carrington, lakini Ten Hag alisema itabidi wachunguzwe kabla ya uamuzi wa kuwatumia kwenye mchezo huo. Alisema Ten Hag.

# Ronaldo atia neno Pepe akitundika daruga



**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo alitoa pongezi kwa mchezaji mwenzake wa muda mrefu wa Ureno, Pepe baada ya beki huyo kutangaza kustaafu soka akiwa na umri wa miaka 41.

Mechi ya mwisho ya Pepe ilikuwa Euro 2024, ambapo Ureno ilifungwa na Ufaransa kwa mikwaju ya penalti katika robo fainali, na akawa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kutokea kwenye michuano hiyo.

Aliichezea Ureno mechi 141, nyuma ya Ronaldo (211) na João Moutinho (146).

Pepe, Ronaldo na Moutinho walikuwa wachezaji wa timu ya Ureno ambayo iliishinda Ufaransa 1-0 kwenye fainali ya Ubingwa wa Ulaya mwaka 2016.

"Hakuna maneno ya kutosha kuelezea jinsi unavyomaanisha kwangu, rafiki," aliandika Ronaldo kwenye mtandao wa X.

"Tulishinda kila kitu, na tulishindwa pia uwanjani, lakini mafanikio makubwa ni urafiki na heshima niliyonayo kwako. Wewe ni wa kipekee kaka yangu, asante kwa mengi."

Pepe pia alitumia misimu 10 akiwa Real Madrid, nane kati ya hizo akiwa na Ronaldo ambapo alishinda mataji matatu ya LaLiga na mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na mataji mawili ya Klabu bingwa ya Dunia.

Pepe alijiunga na timu hiyo ya Hispania mwaka 2007 akitokea Porto, na akarejea katika klabu hiyo ya Ureno mwaka 2019 ambako alibakia hadi mwisho wa soka lake, akishinda mataji manne ya Ligi Kuu nchini humo.

# Buriani Issa Hayatou

**PARIS,** Ufaransa

ISSA Hayatou, kiongozi wa muda mrefu wa soka barani Afrika ambaye aliteuliwa kuwa rais wa muda wa Shirikisho la soka la kimataifa, FIFA, wakati wa mzozo wa rushwa mwaka 2015, amefariki dunia siku ya Alhamisi akiwa na umri wa miaka 77.

Rais wa FIFA, Gianni Infantino alisema katika chapisho lake katika mtandao wa Instagram: "Nimehuzunishwa kusikia kifo cha rais wa zamani wa CAF, rais wa zamani wa FIFA, Makamu wa rais wa FIFA na mjumbe wa Baraza la FIFA Issa Hayatou. Akiwa shabiki wa michezo, alijitolea maisha yake kwa michezo. kwa niaba ya FIFA, rambirambi ziende kwa familia yake, marafiki, wafanyakazi wenzake wa zamani na wote wanaomfahamu, apumzike kwa amani."

Hayatou pia alikuwa mwanachama wa Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki kwa miaka 15, hadi 2016, na alibaki kuwa mwanachama wa heshima.

Alifariki huko Paris wakati jiji hilo likiwa mwenyeji wa michezo ya Olimpiki.

Ingawa alikuwa mkimbiaji bingwa wa kitaifa katika riadha, ilikuwa katika soka ambapo Hayatou alipanda mamlaka na ushawishi kutoka nchi yake ya asili ya Cameroon.

Alichaguliwa kuongoza Shirikisho la Soka Afrika mwaka 1988 na ndani ya miaka minne alikuwa makamu wa rais wa Shirikisho la soka duniani FIFA.

Mwaka 2002, wakati wa msukosuko mkubwa wa kifedha na kisiasa katika FIFA, Hayatou alipingana na rais wa wakati huo Sepp Blatter katika uchaguzi ambao alipoteza licha ya kuungwa mkono huko Ulaya. Matokeo ya 139-56 yalionesha Hayatou alikuwa amepoteza kura kutoka kwa wenzake wa Kiafrika.



## Simba, Yanga hawajamalizana

INATOKA UKURASA 24

Mwanza na Jumamosi ijayo ligi itaendelea kwa michezo miwili kati ya Mashujaa FC dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, huku Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, kutakuwa na mechi nyingine kati ya Namungo dhidi ya Fountain Gate.

Jumapili ijayo, mbali na mechi ya Simba dhidi ya Tabora United, kutakuwa na mechi nyingine kwenye Uwanja wa Sokoine wakati KenGold FC itakapovaana na Singida Big Stars.

## Magoma yamkuta Mahakamani

INATOKA UKURASA 24

ni sababu ya kuikubalia bodi hiyo kufanya marejeo ya shauri hilo.

"Sababu ya nne, baada ya mahakama kupitia kumbukumbu ya shauri namba 187/2022 imebaini kuwa Abeid alijitanabaisha kuwa yeye ni Mwenyekiti wa Bodi na kwamba Fatma Karume alimruhusu amwakilishe mahakamani jambo ambalo hakuwahi kuruhusiwa kufanya hivyo,"

"Abeid hakuwahi kupata idhini kutoka kwa mtu yeyote ya kumsimamia mahakamani na hakuweza kujibu chochote juu ya tuhuma hizi kwa maana hiyo bodi ya wadhamini na Karume hawakuwa na mwakilishi, hivyo walinyimwa haki yao ya kusikilizwa,"alisema

Hakimu huyo, alisema kwa sababu hizo mahakama inaona maombi ya marejeo yana mashiko, kwa hiyo imekubali Bodi ya Wadhamini ya Klabu ya Yanga kufanya hivyo.

"Mahakama imetupilia mbali mwenendo nzima wa maombi namba 187/2022 yaliyofunguliwa na Magoma na wenzake na kuweka kando amri zote zilizotolewa katika hukumu hiyo pamoja na tuzo iliyotolewa Agosti 2,2023,"

"Na kuhusiana na gharama za shauri hili, mahakama inaamuru Magoma, Mwaipopo na Abeid wamlipe muombaji wa maombi ya marejeo ambayo ni Bodi ya Wadhamini wa Klabu ya Yanga,"alisema Hakimu Kiswaga

Ilidaiwa kuwa, Novemba 6, mwaka 2022, watu wawili waliojiita wanachama wa Yanga walifungua shauri ambao ni Juma Ally (Magoma) aliyekuwa mlalamikaji namba moja na Geofrey Mwaipopo ambaye ni mlalamikaji namba mbili na wa tatu ni Jabir Katundu.

Walifungua dhidi ya Baraza la Wadhamini kama mlalamikiwa namba moja, Fatma Karume, Abeid Mohamed Abeid, ambaye ni mlalamikiwa namba tatu.

Alisema walichokuwa wakihitaji ni kuondoka kwa viongozi waliopo sasa madarakani, na mali za klabu na timu wakabidhiwe wao, mwenendo wa shauri hilo ndiyo ambao umetupiliwa mbali.

# FADLU DAVIDS, GAMONDI WAFUNGUKA VIKOSI

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya mchezo wa juzi wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii, makocha wa timu zote yaani Simba na Yanga, Fadlu Davids na Miguel Gamondi mtawaliwa, kila mmoja amefunguka akielezea uwezo wa timu hizo.

Katika mchezo huo wa juzi, Yanga walifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0, bao lililofungwa mwishoni mwa kipindi cha kwanza na kiungo, Max Nzengeli.

Kocha wa Yanga, Gamondi, licha ya kuwasifia wachezaji wake kwa kufuata maelekezo yake, lakini pia alikubali uwezo wa wapinzani wao walioonesha kwenye mchezo huo uliokuwa na upinzani mkubwa.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kutokana na juhudi waliyoifanya katika mchezo huu kwa sasa tunakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo wetu wa fainali dhidi ya Azam FC, lakini siwezi kuacha kuwasifu wapinzani wetu, walitupa kipimo kizuri, ilitulazimu kupambana ili kupata matokeo haya, ulikuwa mchezo mzuri sana," alisema Gamondi.

Alisema, licha ya ushindi huo na uwezo wa wachezaji wake waliouonesha, amebaini makosa kadhaa kwenye kikosi chake ambayo ni lazima ayafanyie kazi.

**"tunasiku chache kabla ya michezo ya Ligi na mashindano ya kimataifa, tutaenda kufanyia kazi mapungufu niliyoyaona ili kukiimarisha zaidi kikosi changu," alisema.**

Kwa upande wake, Kocha wa Simba, Fadlu, alisema licha ya timu yake kupoteza mchezo huo wachezaji wake wameonesha kiwango kizuri.

Alisema timu yake inahitaji muda mchache kuendelea kuzoeana na itafanya vizuri zaidi kwenye michezo ya ligi kuu na mashindano ya kimataifa.

"Timu zote zimeonesha uwezo mzuri katika mchezo huu, wenzetu wamepata nafasi moja wameweza kuitumia lakini bado sijakata tamaa najipanga kwa ajili ya michezo ijayo, nina kikosi kizuri nadhani watu wameona, kuna mambo madogo nayafanyia kazi, tutakuwa imara, imara zaidi," alisema Fadlu.

Alisema amefurahishwa na uwezo wa kila mchezaji wake aliyepata nafasi ya kucheza na kuwataka mashabiki wa timu hiyo kuwa na subira.



Mkurugenzi wa sheria wa klabu ya Yanga, Saimon Patrick (kushoto) na mawakili wenzake, wakitoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana baada ya kushinda maombi ya marejeo ya kesi dhidi ya Juma Magoma na wenzake. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# *Matamasha Mashujaa, Pamba, Fountain Gate leo*

**Na Adam Fungamwango**

UNAWEZA ukasema leo ni 'Jumamosi ya Matamasha', ambapo jumla ya timu nne za Ligi Kuu zinatarajia kufanya matamasha yao kama ilivyokuwa kwa Simba Day na kilele cha Wiki ya Mwananchi.

Kama inavyoeleweka kuwa, matamasha hayo ni maalumu kwa ajili ya kutambulisha wachezaji, burudani na kucheza mechi ya kirafiki na mara nyingi zinakuwa ni timu kutoka nje ya nchi.

Timu ya Mashujaa, yenyewe itakuwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma katika tamasha walilolipa jina la 'Mashujaa Day' ambapo pamoja na burudani kadhaa, itamalizia tamasha hilo kwa kucheza dhidi ya klabu ya Inter Star kutoka Burundi.

Jijini Mwanza, timu ya Pamba FC ambayo imepanda daraja msimu huu, nayo itakuwa na siku yao walioipa jina la 'Pamba Day', ambapo baada ya burudani na kutambulisha wachezaji wake, itakipiga dhidi ya Vital'O ya Burundi

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Pamba Day, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, amesema maandalizi yote ya tamasha hilo yamekamilika, hivyo tunawaomba wakazi wa Mwanza na vitongoji vyake kujitokeza kwa wingi.

Pamba itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya miaka 23, kwani ilishuka daraja mwaka 2001.

Timu ya Fountain Gate yenyewe itafanya tamasha lake kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, mkoani Manyara, ambapo pamoja na shughuli zingine za kiburudani, litahitimishwa kwa kucheza dhidi ya Gor Mahia ya Kenya.

Singida Big Stars nayo siku hiyohiyo, itacheza dhidi ya Agle Noir ya Burundi, Uwanja wa Liti, Singida, na matamasha yote hayo yanafanyika ikiwa imesalia wiki moja tu kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanza kutimua vumbi.

# Michezo

Jumamosi Agosti 10, 2024

Nipashe




Buriani Issa Hayatou UKURASA 22




Kiungo wa Yanga, Stephane Aziz Ki (katikati) akifurahia jambo na mabeki wa Simba, Mohamed Hussein (kulia) na Che Fondoh Malone baada ya mchezo wao wa nusu fainali Ngao ya Jamii juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga walishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Magoma yamemkuta Mahakamani, atakiwa kuilipa Yanga mamilioni

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetupilia mbali mwenendo mzima wa maombi yaliyofunguliwa na Mzee Juma Magoma na wenzake ya kutaka kuondoa uongozi wa Klabu ya Yanga madarakani na pia kuweka kando tozo na amri zote zilizotolewa katika hukumu iliyowapa ushindi wazee hao.

Aidha, Mahakama hiyo imemuaru Magoma, Geofrey Mwaipopo na Abeid Mohamed Abeid wamlipe muombaji ( Bodi ya Wadhamini ya Klabu ya Yanga) gharama za uendeshaji wa shauri hilo.

Uamuzi huo, ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo, wakati akitoa uamuzi wa marejeo ya shauri la maombi namba 187/2022 yaliyoombwa na bodi hiyo kwa madai kuwa, wazee hao hawakuwa na sifa ya kufungua shauri.

Hakimu Kiswaga alisema bodi hiyo iliwasilisha maombi manne ya kuomba kufanya marejeo, ambapo mahakama imekubali matatu na moja imelitupilia mbali kwa madai kuwa halina mashiko kisheria.

Alisema kuwa, sababu ya kwanza ni kwamba, bodi hiyo inadai kuwa Magoma na wenzake walipeleka maombi yao kwenye mahakama ambayo haina mamlaka ya kuyasikiliza ambayo ni Mahakama ya Kisutu.

"Kutokana na maombi yao waliyoyeleta kwenye maombi namba 187/2022 ni wazi yalitakiwa kupelekwa Mahakama Kuu na siyo hapa kwa sababu walikuwa wanalalamika juu ya uhalali wa uwapo wa Bodi ya Wadhamini wa Klabu ya Yanga na uongozi uliopo sasa madarakani,"alisema Kiswaga

Alisema sababu ya pili, Mahakama inaona haina mashiko kwa sababu, ili mahakama iweze kufanya marejeo haipaswi kwenda kuangalia ushahidi, suala la kwamba walitakiwa kutoa kadi za uanachama ili kuhalalisha uanachama wao ni suala la ushahidi.

Pia, alisema sababu ya tatu, Magoma na Mwaipopo walitakiwa kufungua shauri kwa hati ya madai na siyo maombi kama walivyowasilisha wao, jambo ambalo mahakama imeona

ENDELEA UKURASA 23

# Simba, Yanga hawajamalizana

**Na Adam Fungamwango**

### ● ● ● Bodi ya Ligi yawachonganisha tena, kukutana uso kwa uso tarehe...

SIKU moja tu baada ya kumalizika kwa mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii kati ya Simba na Yanga, Bodi ya Ligi, imetoa ratiba ya ligi msimu wa 2024/2025, ikionesha timu hizo zitakutana tena Oktoba 19 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza.

**Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na na bodi hiyo, mchezo huo utakuwa wa mzunguko wa nne wa Ligi Kuu, umepangwa kuchezwa Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, Simba ikiwa ni mwenyeji.**

Hiyo itakuwa fursa nzuri kwa Simba kulipiza kisasi kwani imepoteza mechi zake tatu mfululizo za hivi karibuni dhidi ya watani zao hao, msimu uliopita ilifungwa michezo yote miwili ya Ligi Kuu.

Ilianza kwa kuchapwa mabao 5-1 katika mzunguko wa kwanza mechi iliyochezwa Novemba 5, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, na mchezo wa mzunguko wa pili ikafungwa mabao 2-1, uwanja huo huo, Aprili 20, kabla ya Alhamisi iliyopita kudunguliwa bao 1-0 katika mechi ya Ngao ya Jamii.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi, Simba itafungua dimba la Ligi Kuu, Jumapili ijayo, Agosti 18, dhidi ya Tabora United, mechi ikipigwa Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, huku Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga wakisubiri hadi Agosti 29, watakapoanza ligi kwa kucheza na Kagera Sugar.

Yanga haitocheza mechi ya ligi wiki ya kwanza inayotarajiwa kuanza Ijumaa ijayo kutokana na kuwa kwenye majukumu ya kimataifa, ikitarajiwa kucheza mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika, dhidi ya Vital'O ya Burundi, Agosti 17.

Timu zingine ambazo hazitocheza mechi yoyote ya ufunguzi wa ligi wiki ijayo ni Azam ambayo itacheza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR na itarejea kucheza Ligi Agosti 28 dhidi ya JKT Tanzania, Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam huku Coastal Union inayocheza Kombe la Shirikisho Afrika yenyewe itacheza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Agosti 29 dhidi ya KMC, Uwanja wa KMC, Dar es Salaam.

Simba itacheza mechi yake wiki ijayo kwa sababu haipo kwenye hatua za awali ya mashindano ya kimataifa, itaanzia hatua ya kwanza inayotarajiwa kuanza Septemba.

Ligi Kuu Tanzania Bara itaanza ijumaa ijayo kwa mechi kati ya Pamba Jiji dhidi ya Prisons, Uwanja wa CCM Kirumba,

ENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >